TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA

JAMII ADILIFU NA YENYE UJUZI

# KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA

## MTAALA WA SHULE ZA MSINGI

## GREDI YA 1, 2 NA 3

Chapisho la Kwanza 2017

Chapisho la Pili 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

ISBN: 978-9914-43-071-4
Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

## DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU

Serikali ya Kenya imejitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera ya elimu, mafunzo na utafiti yanatimiza maazimio ya Katiba ya Kenya, 2010, Ruwaza ya Kenya, 2030, Sera ya Mtaala ya Kitaifa ya 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na mikataba ya kieneo na kimataifa ambayo Kenya ni mshirika. Katika kutimiza kauli mbiu ya Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu imefanikiwa kuanzisha utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika viwango vya Chekechea, Shule za Msingi na Shule za Junia.

Utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi unahusisha ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kwamba umefanikiwa. Baada ya kutekelezwa kwa mtaala huu kwa awamu ya kwanza ya miaka mitano, tathmini tamati ya utekelezwaji huu ilifanywa ili kubaini iwapo matokeo yanayotarajiwa kama yanavyoelezewa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) yalifikiwa. Serikali ya Kenya iliunda jopokazi ya Rais ya: *Presidential Working Party on Education Reforms* (PWPER) mwaka wa 2022 kushughulikia masuala nyeti yanayotatiza sekta ya elimu. Jopokazi hii ya rais ilitoa mapendekezo mbalimbali yanayoathiri elimu nchini yaliyochochea kutazamwa upya kwa mtaala wa elimu. Mapendekezo ya jopokazi hii, ripoti za kuangalia utekelezaji wa mtaala, ripoti za tathmini tamati kuhusu utekelezwaji wa elimu ya msingi kiawamu na taarifa kutoka kwa wanaotekeleza mtaala na washikadau wengine zilichangia usawasishaji na kutazamwa upya kwa mtaala wa elimu ya awali. Mtaala uliofanyiwa marekebisho wa shule za msingi unatoa nafasi kwa wanafunzi kukuza uwezo wa kusoma na kuandika pamoja na mbinu za kuweza kuhesabu (*basic literacy and numeracy*) na kuweza kuingiliana na mazingira yao. Wanafunzi wanajenga juu ya umilisi walioupata katika shule za chekechea na pia kuwaandaa kujiunga na shule ya msingi ya juu.

Mtaala unawasilisha Malengo ya Elimu ya Taifa, Matokeo yanayotarajiwa ya kiwango, kauli kiini, matokeo ya kijumla yanayotarajiwa, mada na mada ndogo. Mtaala pia unatoa matokeo maalum yanayotarajiwa, shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa, maswali dadisi yaliyopendekezwa, umilisi wa kimsingi, masuala mtambuko, maadili na pia viwango na vigezo vya kutathmini.

Ni matumaini yangu kwamba mitaala hii itatumiwa na mashirika ya serikali na washikadau wengine kupanga kikamilifu na kutekeleza wa Mtaala wa Kiumilisi.

**HON. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**
**WIZARA YA ELIMU**

## DIBAJI YA KATIBU MKUU

Mwaka wa 2019 Wizara ya Elimu ilizindua utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kupitia mfumo wa ana kwa ana. Daraja ya chini ya Shule za Msingi ni kiwango cha kwanza katika elimu ya msingi baada ya masomo ya Chekechea katika muundo uliotolewa katika ***Basic Education Act of 2013*. Mitaala iliyofanywa upya imejengwa katika msingi wa elimu ya Chekechea. Inawapatia wanafunzi nafasi ya kuingiliana na mazingira yao pamoja na kukuza mbinu za kusoma, kuandika pamoja na kuhesabu. Hii inaoana na ruwaza na mwito wa mageuzi ya mtaala kama inavyoelezwa katika** Mtaala wa Kiumilisi. Kiwango hiki cha elimu ni muhimu katika kuchangia kufikia ruwaza na mwito wa mabadiliko yanayoendelea ya kimtaala kama ilivyoelekezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 kuhusu Katika kuafikia elimu na mafunzo yenye ubora na jumuishi kwa maendeleo endelevu nchini Kenya. Mswada Elekezi huo unaeleza kuhusu kuvuka kutoka mtaala wa Kimafunzo na kuzingatia kukuza vipawa vya kila mwanafunzi

**Mitaala ya shule za msingi daraja ya chini katika juzuu tatu:**
**Juzuu ya kwanza: English Language Activities na Kiswahili Mazoezi ya Lugha.**
**Juzuu ya pili: Indigenous Language Activities na Creative Activities.**
**Juzuu ya tatu: Mathematical Activities, Environmental and Religious Activities.**

Mitaala hii inalenga kukuza umilisi wa mwanafunzi kwa kutoa maelezo yanayooana na mihimili ya Mtaala wa Kiumilisi. Mitaala hii pia inalenga kuelekeza wasomi kwa njia ifaayo na kusaidia ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi kufikia matokeo yanayotarajiwa. Inatoa mapendekezo ya shughuli za ujifunzaji za kimwingiliano ili kufanya ujifunzaji uwe wa kupendeza, kisisimua na kuburudisha.

**DKT. BELIO KIPSANG**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA AWALI NA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

## SHUKRANI

Sheria Nambari 4 ya 2013 (Toleo jipya 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala ya Kenya (KICD) inaipa uwezo Taasisi kukuza Mitaala na vifaa vya msaada kwa mtaala kwa elimu ya msingi na ya vyuo vya Elimu na Mafunzo. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote huhusisha utafiti, ulinganishi wa kimataifa, na uhusishaji mkubwa wa wadau wa elimu. Kupitia kwa mchakato huu wa utaratibu na wa kimashauriano, KICD ilizua wazo la Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (KICD), 2017. Unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Kanuni za Jumuia ya Afrika Mashariki na maelekezo kuhusu shirika la *International Bureau of Education.* *(*IBE) na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SGD).

KICD hufadhiliwa na Serikali ya Kenya ili kutekeleza majukumu na mipangilio ya serikali na sekta ya elimu. Pia, Taasisi hupata misaada kutoka kwa mashirika mengine ya kimaendeleo yanayoangazia miradi teule. Mitaala ya Gredi ya 1-3 imekuzwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Kenya Primary Education Equity in Learning Programme (KPEELP*), chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu. Tuna shukrani nyingi kwa msaada wa serikari kupitia Wizara ya Elimu na washirika wetu wa kimaendeleo kwa sababu ya sera, rasilimari na msaada pia wa kiufundi. Shukrani maalum kwa Waziri wa Wizara ya Elimu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Idara ya Serikali ya Elimu ya Awali na ya Msingi kwa mchango wao.

Ningependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wanaelimu wengine walioshiriki kama wanajopo, sekta mbalimbali za serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali walioshiriki kuandika mitaala hii ya Gredi ya 1-3. Kuhusiana na hili, ningependa kumshukuru Katibu wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Kitaifa la Mitihani (KNEC) kwa msaada wao katika mchakato wa kukuza mitaala hii. Mwisho, nalishukuru baraza la KICD kwa maongozi yake katika ukuzaji wa mitaala. Nawahakikishia waalimu, wazazi na washikadau wengine kuwa, mitaala hii itaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya 1-3 na kuwaandaa wanafunzi vilivyo kujiunga na Gredi za 4-6.



**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO, MBS**
**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU**
**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

## YALIYOMO


DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU ........ iii

DIBAJI YA KATIBU MKUU ........ iv

SHUKRANI ........ v

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ........ vii

MGAO WA VIPINDI ........ ix

MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA YA ELIMU YA MSINGI ........ ix

KAULI KIINI ........ x

MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI ........ x

KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA GREDI YA 1 ........ 1

MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ........ 84

KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA GREDI YA 2 ........ 90

MWONGOZO ULIOPENDEKEZWA WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ........ 178

KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA GREDI YA 3 ........ 184

MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ........ 268

KIAMBATISHO: SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL) ........ 274

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

   a) **Mahitaji ya kijamii**
   Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
   Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
   Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.
   Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
   Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira.**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

## MGAO WA VIPINDI

| | Somo | Vipindi Vilivyopendekezwa |
|---|---|---|
| 1. | Indigenous Language Activities | 2 |
| 2. | Kiswahili Language Activities / Kenya Sign Language Activities | 4 |
| 3. | English Language Activities | 5 |
| 4. | Mathematical Activities | 5 |
| 5. | Religious Education Activities | 3 |
| 6. | Environmental Activities | 4 |
| 7. | Creative Activities | 7 |
| 8. | Pastoral/Religious Instruction Programme | 1 |
| **Total** | | **31** |

## MATOKEO MAALUM YANAYOTARAJIWA YA ELIMU YA MSINGI

Kufikia mwisho wa elimu ya msingi, mwanafunzi aweze:

a) kuwasiliana apasavyo akitumia mbinu za mazungumzo na ishara katika miktadha mbalimbali,
b) kudhihirisha ufahamu wa hali ya juu wa dhana mbalimbali katika kusuluhisha matatizo ya kila siku,
c) kutumia ujuzi wa kijamii, mienendo na maadili ya kidini kwa nia ya kuchangia kukua kwa jamii,
d) kukuza talanta kwa nia ya kujiendeleza na kujifanikisha,
e) fanya maamuzi kutokana na ufahamu wa mambo kama mwananchi wa kitaifa na kimataifa mwenye jamii zenye demokrasia tofauti katika ulimwengu huru,
f) ibua mikakati bunifu inayoweza kuifadhi na kudumisha mazira,
g) kutumia ujuzi wa kidijitali kujifunza na kujifurahisha,
h) kufurahia haja ya umuhimu wa tamaduni nyingi na zenye utajiri kwa nia ya kutegemeana kwa binadamu.

## KAULI KIINI

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na lugha ya mawasiliano katika eneo la Afrika Mashariki na Kati. Wakenya wengi hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Ni muhimu wanafunzi wapate umilisi wa kuwasiliana kwa Kiswahili mapema hasa katika shule za msingi. Somo hili humwezesha mwanafunzi kujenga stadi za kimsingi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Aidha, somo hili humwandaa mwanafunzi kwa mafunzo ya viwango vya juu na baadaye katika ajira.

## MATOKEO YA KIJUMLA YA SOMO LA KISWAHILI

Kufikia mwisho wa kiwango cha chini, mwanafunzi aweze:

a) kusikiliza kwa makini na kuitikia ipasavyo kwa Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano,
b) kuzingatia kanuni za lugha ili kuwasiliana kiubunifu kwa njia ya mazungumzo na maandishi,
c) kujieleza kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali,
d) kusoma kwa ufasaha na kufahamu matini mbalimbali yaliyochapishwa na ya kidijitali na kutumia maarifa anayoyapata katika mazingira tofauti maishani,
e) kutumia hati za kimaandishi na mfumo wa kidijitali kuwasiliana ipasavyo kwa kuzingatia mitindo na miundo husika katika miktadha mbalimbali,
f) kuchangamkia matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa katika mawasiliano ya kila siku.

# KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA
# GREDI YA 1

## 1.0 DARASANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi na maagano,<br>b) kuamkua na kuitikia maamkuzi na maagano ipasavyo ili kufanikisha mawasiliano,<br>c) kuchangamkia maamkuzi na maagano katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua maneno ya maamkuzi (*Hujambo? Hamjambo? Habari? Sijambo, Hatujambo, Nzuri*) na maagano (*Kwaheri, Kwaheri ya kuonana*) kwa kutumia kadi maneno, michoro, chati, mti maneno, kapu maneno n.k. akishirikiana na wenzake,<br>• kusikiliza kifungu kifupi cha hadithi kuhusu maamkuzi na maagano mepesi kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali,<br>• kutambua maamkuzi na maagano yaliyotumiwa katika hadithi aliyoisikiliza akishirikiana na wenzake,<br>• kujadili michoro au picha zenye watu wanaoamkuana na wanaoagana akishirikiana na mwenzake,<br>• kuigiza maamkuzi na maagano (*k.v. Hujambo? - Sijambo; Hamjambo? - Hatujambo; Habari? - Njema/Nzuri; Kwaheri -* | Unatumia maneno gani kuwasalimu na kuwaaga watu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • *Kwaheri ya kuonana*) darasani akishirikiana na mwenzake au katika kikundi kwa kuzingatia umoja, upendo na heshima kwa wenzake,<br>• kueleza wenzake kuhusu maamkuzi na maagano aliyojadili na mzazi au mlezi wake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi, kusikiliza na kutoa maoni yake kikamilifu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia maamkuzi na maagano.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojifunza maamkuzi na maagano yanayotumiwa katika jamii yake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza maamkuzi na maagano mbalimbali.

**Maadili:**

- Uzalendo: mwanafunzi anapojadili na mzazi au mlezi kuhusu maamkuzi na maagano katika jamii yake.
- Amani: mwanafunzi anapoamkuana na wenzake kwa utulivu.
- Uadilifu: mwanafunzi anapomwamkua mwalimu, mzazi au mlezi ifaavyo kwa heshima.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotumia maamkuzi na maagano katika jamii anaimarisha mahusiano ya kijamii.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maamkuzi na maagano aliyojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Usomaji Mwafaka**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua namna ifaayo ya kuketi anaposoma,<br>b) kutambua jinsi ya kushika kitabu ipasavyo anaposoma,<br>c) kuelekeza macho kutoka kushoto hadi kulia na kutoka juu ya ukurasa hadi chini anaposoma,<br>d) kuonea fahari usomaji mwafaka maishani. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua namna ya kuketi anaposoma (*k.v. kutoinama sana, kuketi wima, kutoning'iniza miguu*) kutoka kwenye picha, michoro, magazeti, vitabu, vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kufanya mazoezi ya kuketi ipasavyo anaposoma,<br>● kutambua jinsi ya kushika kitabu ipasavyo kwa kutazama picha au michoro kwenye magazeti, chati, mabango, vitabu, vifaa vya kidijitali n.k. akishirikiana na wenzake,<br>● kufanya mazoezi ya kushika kitabu ipasavyo anaposoma,<br>● kuelekeza macho kutoka kushoto hadi kulia na kutoka juu ya ukurasa hadi chini akiongozwa na mwalimu,<br>● kutazama picha mbalimbali zinazotoka kushoto kwenda kulia na juu kwenda chini,<br>● kufanya mazoezi ya kufungua kurasa za kitabu ipasavyo, | Je, unazingatia mambo gani unaposoma? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>kumsomea mzazi au mlezi kwa kuzingatia namna ifaayo ya kuketi na kushika kitabu.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kikundi kuonyesha jinsi ya kuketi ifaavyo, kushika kitabu na kuelekeza macho ipasavyo ili kusoma.</li><li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama namna ifaayo ya kutekeleza shughuli ya kusoma.</li><li>Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi kuonyesha jinsi ya kusoma ifaavyo.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<ul><li>Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kusoma katika kikundi.</li><li>Amani: mwanafunzi anapoonyesha utulivu akishiriki katika shughuli za kikundi.</li><li>Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki wakati wa shughuli za kikundi.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<ul><li>Haki za watoto: mwanafunzi anajitambua anapojifunza namna ya kuketi, kushika kitabu na kuelekeza macho ipasavyo anaposoma.</li><li>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutazama picha au michoro.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uwezo wa matayarisho ya usomaji mwafaka yaliyoshughulikiwa katika masomo ya English Language Activities na Indigenous Language.</td></tr>
</table>

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Uandishi Bora**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua namna ifaayo ya kuketi anapoandika,<br>b) kuketi ifaavyo wakati wa kuandika,<br>c) kutambua jinsi ya kushika kalamu anapoandika,<br>d) kuandika kutoka kushoto hadi kulia kwa hati nadhifu,<br>e) kuonea fahari uandishi mwafaka maishani. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama picha zinazoonyesha jinsi ya kuketi na kushika kalamu katika vitabu au katika kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua jinsi ya kuketi ipasavyo wakati wa kuandika kutoka kwenye picha,<br>● kuketi ipasavyo wakati wa kuandika,<br>● kumwonyesha mwenzake jinsi ya kuketi wakati wa kuandika,<br>● kutambua namna ya kushika kalamu kutoka kwenye picha, michoro, magazeti, vitabu, vifaa vya kidijitali n.k akishirikiana na wenzake,<br>● kushika kalamu na kuidhibiti ipasavyo,<br>● kuwaonyesha wenzake jinsi ya kushika kalamu ipasavyo wakati wa kuandika,<br>● kuandika (*kwa mfano kuchora kifaa cha darasani kama vile kiti, kitabu, kalamu, meza*) kwa kushika kalamu ipasavyo na kuidhibiti,<br>● kuwapa wenzake kazi yake waipitie ili waitolee maoni. | Je, ni mambo gani unapaswa kuzingatia wakati wa kuandika? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowaeleza wenzake kuhusu namna ya kuketi na kushika kalamu na kisha kuwasikiliza wakitoa maoni yao.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutazama jinsi ya kuketi na kushika kalamu ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi nyumbani kutazama video kuhusu jinsi ya kuketi na kushika kalamu ipasavyo wakati wa kuandika.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za matayarisho ya kuandika na kuheshimu maoni yao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapobadilishana kazi na wenzake ili wasahihishiane na kutoleana maoni.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kuonyeshana jinsi ya kuketi.

**Masuala mtambuko:**

Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anajitambua anapojifunza namna ya kuketi, kushika kalamu na kuandika ipasavyo kutoka kushoto hadi kulia

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi bora dhana hii katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Matumizi ya Mimi na Sisi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno **mimi** na **sisi** katika sentensi alizopewa,<br>b) kutumia maneno **mimi** na **sisi** ipasavyo katika sentensi alizopewa,<br>c) kufurahia kutumia maneno **mimi** na **sisi** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza wimbo unaotumia maneno **mimi** na **sisi** kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma sentensi fupi zilizoandikwa kwa kutumia maneno **mimi** na **sisi** akishirikiana na wenzake,<br>● kujaza mapengo kwa kutumia **mimi** na **sisi,**<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizokamilisha kwa kujaza nafasi akitumia **mimi** na **sisi** ili ampe maoni yake. | Maneno **mimi** na **sisi** hutumiwa kwa maana gani katika mawasiliano? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kutoa mifano ya sentensi zenye matumizi ya maneno **mimi** na **sisi**.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya maneno **mimi** na **sisi** darasani.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya maneno **mimi** na **sisi**.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia maneno **mimi** na **sisi** ifaavyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kuigiza matumizi ya maneno **mimi** na **sisi**.<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli ya kikundi.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapotumia maneno **mimi** na **sisi** katika mawasiliano kwa kutunga sentensi zenye maadili. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapojitambua na kutambua wenzake anapotunga sentensi zinazohusisha maneno mimi na sisi.<br>● Elimu ya mazingira: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nafsi na dhana inayofunzwa katika somo la *English Language Activities.* |

## 2.0 FAMILIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Matamshi Bora**<br><br>**Sauti:**<br>*(/m/, /a/, /u/, /k/, /t/ /l/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika matini,<br>b) kutamka sauti lengwa ipasavyo ili kuimarisha mazungumzo,<br>c) kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo,<br>d) kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa,<br>e) kuchangamkia nafasi ya matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa katika kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia teknolojia (*k.v. papaya*) kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kusikiliza mwalimu au mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa,<br>● kutamka sauti pamoja na mwalimu,<br>● kutamka sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali (k.*v. kinasasauti au rununu)* akishirikiana na wenzake,<br>● kutamka silabi za sauti lengwa alizosikiliza akishirikiana na wenzake, | Unaweza kutamka sauti zipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali,<br>• kutamka maneno ya sauti lengwa ifaavyo akishirikiana na wenzake,<br>• kumtamkia mzazi au mlezi maneno yenye sauti lengwa ipasavyo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunza matamshi bora ya sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka sauti lengwa na silabi za sauti lengwa ipasavyo.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujifunza matamshi yafaayo ya sauti lengwa na silabi za sauti lengwa
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamkiana na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa.
- Haki za kijamii: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake kutoka jamii mbalimbali.

**Masuala mtambuko:**

- Mahusiano ya kifamilia: mwanafunzi anapotaja majina yanayoundwa na sauti lengwa na yanayohusiana na suala lengwa k.v. kaka, mama.
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake au na mgeni mwaalikwa kutamka sauti lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora na dhana hii katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities..*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>**Sauti:** (/m/, /a/, /u/, /k/, /t/, /l/)<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>d) kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno yenye sauti lengwa, kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 5 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi*) akishirikiana na wenzake),<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijtali akishirikiana na wenzake, | 1. Je, ni maneno yapi unayojua kusoma?<br>2. Je, kwa nini ni muhimu kusoma kwa sauti inayosikika? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>ili kufanikisha mawasiliano.</td><td>● kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu kutambua silabi za sauti lengwa katika shughuli za kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma silabi na maneno yenye sauti lengwa.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi wake kutambua na kusoma silabi na maneno yenye sauti lengwa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>Mahusiano ya kifamilia:  mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasha na dhana hii katika masomo ya English Language Activities na Indigenous Language Activities.</td></tr>
</table>

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati nadhifu - Herufi kubwa**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maumbo ya herufi kubwa,<br>b) kuandika herufi kubwa ipasavyo kwa kuzingatia maumbo yake,<br>c) kufurahia kuandika herufi kubwa ipasavyo kwa kuzingatia maumbo yake. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kushirikiana na wenzake kutambua herufi kubwa kwenye kitabu, kadi maneno, chati au vifaa vya kidjitali,<br>● kutambua maumbo ya herufi kubwa akiwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwa kutumia kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake katika kikundi kuandika herufi kubwa ipasavyo,<br>● kuandika herufi kubwa ipasavyo kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kutathmini herufi kubwa alizoandika. | Je, ni herufi gani kubwa unazojua kuandika? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kutambua maumbo ya herufi kubwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika herufi kubwa akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi wake kuandika herufi kubwa akiwa nyumbani kwa kuzingatia maumbo yafaayo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika herufi kubwa ipasavyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kutathmini herufi kubwa alizoandika. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anapojitahidi kuandika herufi kubwa kwa kuzingatia maumbo yake, ukakamavu wake unajengeka.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapowathamini wenzake na kushirikiana katika shughuli za kikundi |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya uandishi wa herufi kubwa na dhana kama hii inayoshughulikiwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Majina**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>b) kuandika majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kuzungumzia vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua majina ya vitu katika mazingira yake kwa kutazama vitu halisi, picha au vifaa vya kidijitali *k.v. vifaa vya nyumbani*,<br>● kutaja majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kuimba wimbo unaotaja vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma majina ya vitu katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>● kuambatanisha michoro na majina ya vitu katika mazingira yake akishirikiana na wenzake. | Je, ni vitu gani hupatikana katika mazingira ya darasani na nyumbani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu katika kutambua majina ya vitu katika mazingira yake.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotaka kujua majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yake.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutaja majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kutaja majina ya vitu kwenye mazingira yake katika umoja na wingi.<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Uzalendo: mwanafunzi anapoimba wimbo unaotaja vitu katika mazingira yake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Utunzaji wa mazingira: mwanafunzi anapoandika majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yake katika umoja na wingi<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua umoja na wingi wa vitu katika mazingira yao. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya umoja na wingi kama inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

## 3.0 TARAKIMU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Adabu na Heshima**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya adabu na heshima yanayotumiwa katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maneno ya adabu na heshima katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya adabu na heshima katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno ya heshima (*asante, pole, tafadhali*) kutoka kwenye chati, kadi maneno, mti maneno, kitabu n.k akishirikiana na wenzake,<br>● kutazama michoro mbalimbali na kujadili neno linalofaa kutumiwa katika shughuli husika (*k.v. mtu akipokea zawadi, mtu akitaka kupishwa apite*) akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza mazungumzo (*k.v. kutoka kwa wanafunzi wenzake, kifungu katika kifaa cha kidijitali*) kisha kutambua maneno ya adabu na heshima yaliyotumika,<br>● kuigiza mazungumzo mafupi yanayotumia maneno ya heshima wakiwa na wenzake, | Je, tunaweza kuonyesha heshima na adabu kwa wenzetu kwa kufanya nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuzungumza na mzazi au mlezi huku wakitumia maneno ya heshima yanayotumiwa katika jamii na kuambatanisha na hisia zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana kikamilifu na wenzake katika kikundi kujadili matumizi ya maneno ya adabu na heshima.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunza matumizi ya maneno ya adabu na heshima.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapozungumza na mzazi au mlezi kwa kutumia maneno ya adabu na heshima kutoka katika jamii yake.
- Uraia: mwanafunzi anapojua kutumia maneno ya adabu na heshima ipasavyo ili kuimarisha mahusiano katika jamii.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali ambavyo anatumia kujifunzia maneno ya adabu na heshima.
- Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano ya kawaida.
- Upendo: mwanafunzi anapotangamana na wenzake bila kuzozana katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu kuonyesha heshima kwa wenzake na jamii.

**Uhusiano na masomo mengine**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya maneno ya adabu na heshima na masomo ya *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities* kwa sababu masomo haya hufundisha maneno haya.

Somo la *Mathematics Activities* pia linazungumzia dhana ya tarakimu.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha ufahamu chenye maneno 6-12 kuhusu suala lengwa na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nano, tisa, kumi)* akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kujibu maswali kutokana na kifungu alichokisoma,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kumweleza mzazi au mlezi kuhusu tarakimu alizojifunza. | Je, unajua hadithi kuhusu nini? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kuhesabu nambari moja hadi kumi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutazama na kusikiliza wimbo kuhusu tarakimu.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuhesabu nambari kuanzia moja hadi kumi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuhesabu tarakimu na kueleza ujumbe wa kifungu.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kutoa maoni yao katika kikundi wanapojadili ujumbe katika kifungu.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya pesa: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufasaha na kama inavyofanywa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>Somo la *Mathematics Activities* pia linazungumzia dhana ya tarakimu. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Hati Nadhifu** ***Herufi Ndogo*** <br><br> **(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maumbo ya herufi ndogo katika maandishi,<br>b) kuandika herufi ndogo kwa kuzingatia maumbo yake,<br>c) kufurahia kuandika herufi ndogo ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maumbo ya herufi ndogo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kutambua herufi ndogo kwenye kitabu, chati au chombo cha kidjitali,<br>● kuandika herufi ndogo ipasavyo kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kutambua maumbo ya herufi ndogo kwenye chati, kitabuni, au chombo cha kidjitali,<br>● kushiriki kuimba nyimbo kuhusu herufi ndogo,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi herufi alizoandika ili azitolee maoni. | Je, unazingatia nini ili kuandika kwa hati nadhifu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua herufi ndogo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidjitali.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika herufi ndogo akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotumia herufi ndogo kuandika katika mazingira tofauti na darasa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika herufi ndogo ipasavyo. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi huku akiheshimu maoni yao.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika herufi ndogo ipasavyo kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kutambua herufi ndogo kwenye kitabu, chati au chombo cha kidjitali. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anapojitahidi kuandika herufi kubwa kwa kuzingatia maumbo yake, ukakamavu wake unajengeka. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha kuanduika hati nadhifu na vile inavyofanywa katika masomo ya *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>Somo la *Mathematics Activities* pia linazungumzia dhana ya tarakimu. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Matumizi ya Huyu na Hawa**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **huyu** na **hawa** kutokana na picha,<br>b) kutumia **huyu** na **hawa** ipasavyo katika mazungumzo,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **huyu** na **hawa** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **huyu** na **hawa** katika picha,<br>● akiwa kwenye kikundi kutumia **huyu** na **hawa** *k.v. Mwanafunzi huyu - wanafunzi hawa,*<br>● kutunga sentensi zinazojumuisha matumizi ya **huyu** na **hawa,**<br>● kusoma sentensi zinazojumuisha matumizi ya **huyu** na **hawa,**<br>● kumtungia mwenzake sentensi kwa kutumia **huyu** na **hawa** katika kikundi,<br>● kujaza nafasi katika daftari kwa kutumia **huyu** na **hawa**. | Maneno **huyu** na **hawa** hutumikaje katika mawasiliano? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutunga sentensi akitumia **huyu** na **hawa**.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuburura majibu sahihi na kuyatia kapuni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutumia **huyu** na **hawa** ipasavyo katika sentensi.

| |
|---|
| ● **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kufanya zoezi huku akizingatia utunzaji unaofaa.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutumia **huyu** na **hawa**.<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapowatungia wenzake katika kikundi sentensi zenye maadili kwa kutumia **huyu** na **hawa**. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Uongozi na utawala mwema: mwanafunzi anapowaongoza wenzake kutunga sentensi katika kikundi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya huyu na hawa na matumizi ya vipashio vya kisarufi katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>Somo la *Mathematics Activities* pia linazungumzia dhana ya tarakimu. |

## 4.0 SIKU ZA WIKI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora**<br>*Sauti: (/n/, /o/, /w/, /e/, /i/, /h/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika matini,<br>b) kutamka sauti lengwa ipasavyo ili kuimarisha mazungumzo,<br>c) kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo,<br>d) kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa,<br>e) kuchangamkia nafasi ya matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa katika kadi maneno, chati, mti maneno au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kutumia teknolojia (*k.v. papaya*) kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>• kusikiliza mwalimu au mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>• kutamka sauti pamoja na mwalimu,<br>• kutamka sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali k.*v.* | Ni sauti zipi unazojua kutamka vizuri? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *kinasasauti na rununu* kisha kutamka silabi za sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakisomwa na mwalimu kisha kutamka maneno hayo,<br>• kumtamkia mzazi au mlezi sauti alizojifunza. | |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka sauti lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunza matamshi bora ya sauti lengwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutamka sauti lengwa na silabi ipasavyo. | | | | |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujifunza matamshi ya sauti lengwa, silabi na maneno ya sauti lengwa.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamkiana na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa.<br>● Haki za kijamii: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake kutoka jamii mbalimbali. | | | | |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapotamka maaneno yenye sauti lengwa ipasavyo katika mawasiliano. | | | | |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora katika Kiswahili na yale yanayofanywa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* | | | | |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali dadisi lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti: (/n/, /o/, /w/, /e/, /i/, /h/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti<br>d) kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo<br>e) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa *(/n/, /o/, /w/, /e/, /i/, /h/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 15 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi*) akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijtali akishirikiana na wenzake, akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti, | Je, unaweza kusoma silabi zipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kutambua sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kwa kuzingatia sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusoma kwa ufasaha.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kusoma na kuheshimu maoni ya wenzake kuhusu usomaji wake.

**Masuala mtambuko:**

Haki za watoto: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kusoma kifungu hadi wamalize wakiwemo wale wasiosoma kwa kasi.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sauti na vile inavyofanywa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali dadisi lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi baina ya herufi katika maneno,<br>b) kuandika maneno kwa kuunganisha silabi,<br>c) kufurahia kuandika maneno kwa kuzingatia nafasi ifaayo baina ya herufi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kuonyesha nafasi baina ya herufi zinazounda maneno kwenye kitabu, chati au chombo cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake katika vikundi kutambua nafasi baina ya herufi katika maneno,<br>● kuandika daftarini maneno kwa kuunganisha silabi akizingatia nafasi ifaayo baina ya herufi zinazounda maneno. | Je, kwa nini tunafaa kuandika kwa hati nadhifu? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika shughuli za kikundi kutambua nafasi baina ya herufi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika maneno kwa kuzingatia nafasi ifaayo baina ya herufi kwa kutumia kifaa cha kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nafasi baina ya herufi katika maneno.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya shughuli ya kikundi kwa pamoja. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za kikundi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha kuandika hati nadhifu na vile inavyofanywa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>Somo la *Mathematics Activities* pia linazungumzia dhana ya tarakimu. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na Wingi wa Majina**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>b) kutumia majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kuzungumzia vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua majina ya vitu katika mazingira yake ya darasani kwa kutazama vitu halisi, picha au vifaa vya kidijitali,<br>● kuimba wimbo unaotaja vitu katika mazingira yake,<br>● kusoma majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi,<br>● kumzungumzia mzazi au mlezi wake kuhusu vitu katika mazingira ya nyumbani kwa kutumia majina yafaayo katika umoja na wingi. | Je, ni vitu gani vya darasani unavyoweza kutaja katika umoja na wingi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutambua vitu katika mazingira yake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojitahidi kujua majina ya vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia majina ya vitu katika umoja na wingi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutumia umoja na wingi.<br>● Uadilifu: mwanafunzi anapotumia umoja na wingi katika mawasiliano kwa kutunga sentensi zenye maadili. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotaja vitu katika mazingira yake kwa umoja na wingi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sarufi katika kiswahili na inavyofanywa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

## 5.0 MIMI NA WENZANGU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza**<br>*Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati wa suala lengwa katika kifungu,<br>b) kutunga sentensi sahihi akitumia msamiati uliotumiwa,<br>c) kusikiliza kifungu anachosomewa cha maneno kati ya 15-20 na kupata ujumbe,<br>d) kujibu maswali kuhusu hadithi aliyosikiliza,<br>e) kuchangamkia kusikiliza kifungu ili kujenga ari ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● Kusikiliza kifungu cha maneno kati ya 15-20 kikisomwa na mwalimu au kupitia vifaa vya kiteknolojia<br>● kushirikiana na wengine kujadili picha zilizojumuishwa kwenye hadithi,<br>● kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi,<br>● kuthibitisha utabiri wake baada ya kusikiliza hadithi,<br>● kutunga sentensi akitumia msamiati uliotumika kwenye hadithi,<br>● kujibu maswali kutokana na kifungu,<br>● kujadiliana kuhusu hadithi waliyosomewa katika kikundi. | 1. Unatarajiwa kufanya nini unaposomewa hadithi?<br>2. Unawezaje kupata ujumbe katika kifungu cha hadithi unachosomewa? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili picha katika hadithi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposikiliza kifungu kikisomwa.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofikiria maana ya msamiati na kuutumia katika sentensi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusikiliza na kujadiliana.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojibidiisha kusikiliza kifungu na kujibu maswali. |
| **Masuala mtambuko**<br>• Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili picha kwenye kifungu. |
| **Uhusiano na masomo mengine**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha ufahamu wa kusikiliza na ule unaofunzwa katika somo la *English Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** *Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua msamiati kuhusu suala lengwa (*k.v. mimi, wenzangu*) kutoka kwenye kadi maneno, chati, mti maneno, kapu maneno akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 13-16 kuhusu suala lengwa na kutambua msamiati wa suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kumweleza mzazi au mlezi kuhusu ujumbe aliopata kutokana na kifungu alichosoma. | Ni mambo gani unayoweza kujifunza katika hadithi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi kutambua ujumbe katika kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi wake kusoma ufahamu kuhusu suala lengwa na kueleza ujumbe.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi kujadili picha na ujumbe katika kifungu.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposoma kifungu na kumweleza mzazi au mlezi ujumbe aliopata.

**Masuala mtambuko:**

Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufahamu katika somo hili na ule unaofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Matumizi ya Kikomo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya kikomo katika maandishi,<br>b) kuandika alama ya kikomo ifaavyo katika daftari,<br>c) kutumia ipasavyo alama ya kikomo katika sentensi,<br>d) kufurahia kutumia alama ya kikomo ipasavyo katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua alama ya kikomo (.) katika sentensi kitabuni, kwenye chati au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kuandika sentensi daftarini au kutumia kifaa cha kidijitali kisha aweke alama ya kikomo,<br>• kutumia alama ya kikomo ipasavyo mwishoni mwa sentensi akishirikiana na wenzake,<br>• kumwonyesha mzazi au mlezi alama ya kikomo na kuitumia ipasavyo katika sentensi. | Alama gani zinazotumika katika kuandika sentensi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua alama ya kikomo na kuitumia katika sentensi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotambua alama ya kikomo katika maandishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia alama ya kikomo ipasavyo kuandika sentensi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika katika kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Kujitambua: mwanafunzi anapotumia alama ya kikomo kwa usahihi na kuwaonyesha wenzake. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya alama ya kikomo na jinsi inavyotumika katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Matumizi ya -angu na -etu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-angu** na **-etu** katika miktadha mbalimbali,<br>b) kutumia **-angu** na **-etu** katika mazungumzo kwa ufasaha ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **-angu** na **-etu** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua matumizi ya **-angu** na **-etu** kwa kurejelea vitu katika mazingira yake,<br>• kuigiza matumizi ya **-angu** na **-etu** akiwa na wenzake katika kikundi kwa kutumia vitu anavyomiliki k.v. *kitabu changu – vitabu vyetu; rafiki yangu - marafiki zetu,*<br>• kusoma sentensi zinazotumia maneno **- angu** na **-etu,**<br>• kukamilisha sentensi zenye matumizi ya **-angu** na **-etu,**<br>• kujaza nafasi kwa kutumia **-angu** na **-etu.** | Je, ni maneno gani unayotumia kuonyesha kuwa kitu ni chako au ni chenu? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kujadili matumizi ya **-angu** na **-etu**.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotumia **-angu** na **-etu** katika mawasiliano.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **-angu** na **-etu**.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuigiza matumizi ya **-angu** na **-etu**.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wakati wa shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **-angu** na **-etu** akiwa na wenzake katika kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma sentensi kuhusu suala lengwa.<br>● Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowasiliana na wenzake kwa ufasaha akitumia **-angu** na **-etu**. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi dhana ya -angu na -etu na vipashio vya kisarufi vinavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

## 6.0 MWILI WANGU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Sauti: (/s/, /b/, /y/, /z/, /g/, /d/)*<br><br>**(vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kadi maneno,<br>b) kutamka sauti lengwa ipasavyo ili kuimarisha mazungumzo,<br>c) kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo,<br>d) kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa,<br>e) kuchangamkia nafasi ya matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kushiriki katika kutambua sauti lengwa katika kadi maneno,<br>● kusikiliza matamshi ya sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka sauti lengwa akiwa na mwalimu kisha akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali k.v. kinasasauti na rununu,<br>● kutamka silabi alizozisikiliza ipasavyo akishirikiana na wenzake,<br>● kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa akishirikiana na wenzake, | Ni sauti zipi unazojua kutamka? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka sauti lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunza matamshi ya sauti lengwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti na silabi za sauti lengwa. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamkiana na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa.<br>● Haki za kijamii: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake kutoka jamii mbalimbali.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamkiana na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa kwa utulivu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Usafi wa kibinafsi: mwanafunzi anapotamka maneno ya sauti lengwa kuhusu suala lengwa k.v. usafi, sabuni na bafu. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora katika somo la Kiswahili na vile inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia sehemu za mwili. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br>*Sauti: (/s/, /b/, /y/, /z/, /g/, /d/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa<br>c) kwa kuzingatia matamshi bora,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa<br>e) kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>f) kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>g) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa *(/s/, /b/, /y/, /z/, /g/, /d/)* katika kifungu Chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatiakiwango kifaacho cha sauti akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno yenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo *(maneno 20 kwa dakika na kuzingatia viakifishi)* akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, nk akishirikiana na wenzake,<br>● kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kwa sauti inayosikika, | Je, ni kwa nini unafaa kutamka maneno vizuri unaposoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kutambua sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia sauti lengwa.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kusoma na kuheshimu maoni ya wenzake kuhusu usomaji wake.

**Masuala mtambuko:**

- Usafi wa kibinafsi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.
- Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya sauti za herufi kama inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Tahajia Imla**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yasiyozidi silabi tatu kutokana na suala lengwa,<br>b) kuandika kwa usahihi maneno yasiyozidi silabi tatu kwa kuunganisha silabi kuunda neno,<br>c) kufurahia kuandika maneno kwa usahihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yasiyozidi silabi tatu kutokana na suala lengwa kwa kusomewa na mwalimu au katika kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yasiyozidi silabi tatu ya kiwango chake yakisomwa na mwalimu au kutoka kwa kifaa cha kidijitali (*k.v radio*) na kuyaandika,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika maneno yasiyozidi silabi tatu ya kiwango chake, kwa kuunganisha silabi kuunda neno,<br>● kuyakosoa maneno aliyoyaendeleza visivyofaa kwa kushirikiana na wenzake. | Je, ni maneno gani ya silabi tatu unayajua? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kupitia kazi ya imla.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kutumia kifaa cha kidijitali kusikiliza maneno yasiyozidi silabi tatu.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofaulu kuandika maneno aliyosomewa yasiyozidi silabi tatu kwa usahihi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kuandika maneno yasiyozidi silabi tatu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Usafi wa mtu binafsi: mwanafunzi anapoandika maneno kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana kuandika imla kama inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia sehemu za mwili. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya -zuri na – baya**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya-**zuri** na-**baya** katika kifungu,<br>b) kutumia **-zuri** na **-baya** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **-zuri** na **-baya** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **-zuri** na **-baya** kwa kurejelea vitu katika mazingira yake,<br>● kutumia **-zuri** na **-baya** akiwa na wenzake katika kikundi kurejelea vitu katika mazingira yake,<br>● kusikiliza matumizi ya **-zuri** na **-baya** kwa kutumia kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma sentensi zinazotumia maneno **- zuri** na **-baya,**<br>● kukamilisha sentensi zenye matumizi ya **-zuri** na **-baya,**<br>● kujaza mapengo kwa kutumia **- zuri** na **-baya,**<br>● kumtajia mzazi au mlezi vitu nyumbani kwa kutumia **-zuri** na **- baya**. | Je, ni maneno gani unayotumia kuelezea vitu vinavyokupendeza au visivyokupendeza? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia **-zuri** na-**baya** akiwa na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza matumizi ya-**zuri** na **-baya**.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia **-zuri** na **-baya.**
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotumia **-zuri** na **-baya.**

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kutumia anapotumia **-zuri** na **-baya.** |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Afya na usafi: mwanafunzi anaposoma sentensi kuhusu suala lengwa.<br>• Mahusiano ya jamii: mwanafunzi anapotunga sentensi akiwa na wenzake kurejelea vitu katika mazingira yake. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi na jinsi inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira. |

## 7.0 USAFI WA MWILI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi yanayotolewa darasani,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani,<br>c) kubainisha maagizo yanayopaswa kufuatwa katika mazingira yake,<br>d) kuthamini umuhimu wa maagizo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maagizo kwa kutazama video ya maagizo,<br>● kutoa na kufuata maagizo (*kama vile simama*, *keti, andika na chora*) akiwa na wenzake katika kikundi,<br>● kueleza kuhusu maagizo yafaayo na yasiyofaa kufuatwa,<br>● kushiriki katika mazungumzo ya matokeo ya kufuata na kutofuata maagizo,<br>● kuimba na kuigiza nyimbo zinazohusu maagizo. | Ni maagizo yapi yanayotakiwa kufuatwa na yasiyotakiwa kufuatwa katika mazingira tofauti? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika kutoa na kuitikia maagizo ipasavyo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia maagizo.

| |
|---|
| • Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojifunza maagizo yanayotumiwa katika jamii yake.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapotambua na kufuata maagizo yafaayo. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapofuata maagizo na kuheshimu nafasi za wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapotoa na kufuata maagizo yafaayo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Afya na usafi: mwanafunzi anapotoa au kufuata maagizo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maagizo na kama inavyofunzwa katika masomo haya ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali dadisi lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 17-22- kuhusu suala lengwa na kutambua msamiati wa suala<br>● lengwa (*mimi*, *wenzangu*) akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua msamiati kuhusu suala lengwa (*k.v. mimi*, *wenzangu*, *oga*, *nawa osha*, *maji*, *sabuni*) kutoka kwenye kadi maneno, chati,<br>● mti maneno, kapu maneno akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kumweleza mzazi au mlezi kuhusu ujumbe aliopata kutokana na kifungu alichosoma. akishirikiana na wenzake, | Je, unapenda kusoma kuhusu nini? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika kikundi kutabiri kwa kutazama picha na kusoma hadithi.<br>● Uwazaji kwa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotabiri yatakayotokea katika hadithi kwa kuzingatia picha.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapowaeleza wenzake ujumbe aliopata kutokana na kifungu.<br>● Amani: mwanafunzi anapowaeleza wenzake kwa utulivu ujumbe aliopata kutokana na kifungu alichosoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika shughuli za kikundi.<br>● Afya na usafi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana kusoma kwa ufahamu katika Kiswahili na vile inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira. |

<table>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo Maalum Yanayotarajiwa</th><th>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</th><th>Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa</th></tr>
<tr><td>7.3<br>Kuandika</td><td>7.3.1<br>Kuandika maneno ipasavyo<br><br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotokana na suala lengwa,<br>b) kuandika maneno yanayohusu suala lengwa kwa kuunganisha silabi ili kuunda neno,<br>c) kufurahia uandishi wa maneno katika mawasiliano.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno mepesi yanayotokana na suala lengwa (k.v : oga, nawa, osha, maji, sabuni),<br>● kuandika maneno yanayotokana na suala lengwa daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali kwa kuunganisha silabi kuunda neno akishirikiana na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili na kurekebisha makosa katika maandishi yake.</td><td>1. Ni maneno gani unayoweza kuandika kwa kuunganisha silabi?<br>2. Kwa nini ni muhimu kujifunza kuandika?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika maneno kwa kuunganisha silabi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika maneno.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofaulu kuandika maneno ipasavyo.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika maneno kuhusu suala lengwa.</td></tr>
</table>

| |
|---|
| **Masuala mtambuko:**<br>• Afya na usafi: mwanafunzi anapoandika maneno kuhusu suala lengwa.<br>• Matumizi yafaayo ya vitu nyumbani: mwanafunzi anapojadili kuhusu matumizi ya vitu vya kudumisha usafi k.v. sabuni, maji na nguo. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana kuandika katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Ukanushaji**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja na wingi katika vifungu,<br>b) kutumia ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja na wingi katika kifungu kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja na wingi katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutenda vitendo atakavyoagizwa na mwalimu kwa kuashiria nafsi ya kwanza umoja,<br>• kutenda vitendo vyake mwenyewe na kusema anachokifanya,<br>• kutambua ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja,<br>• kushirikiana na wenzake katika kikundi kukanusha sentensi katika nafsi ya kwanza umoja,<br>• kukamilisha sentensi zinazoashiria ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja kwa kuelekezwa na mwalimu,<br>• kusikiliza sentensi kwa kutumia kifaa cha kidijitali zilizokanushwa akielekezwa na mwalimu. | 1. Unafanya nini sasa?<br>2. Kama haukufanya mambo uliyotaja ungesemaje? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutunga sentensi akiwa na wenzake katika kikundi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anpofikiria kuhusu sentensi atakazotunga akitumia nafsi ya kwanza na namna ya kuzikanusha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza sentensi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika shughuli za kikundi wanapotungiana sentensi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapofanya zoezi kwa kutumia kifaa cha kidijitali na kukitunza ipasavyo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Afya na usafi: mwanafunzi anapotunga sentensi kwa kutumia msamiati wa suala lengwa.<br>● Matumizi yafaayo ya vitu nyumbani: mwanafunzi anapotumia maneno kuhusu vitu vya kudumisha usafi k.v. sabuni, maji na nguo. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ukanusho na jinsi inavyofunzwa katika *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la E*nvironmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira. |

## 8.0 VYAKULA VYETU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Matamshi bora**<br><br>*Sauti: (/j/, /r/, /p/, /f/, /v/, /sh/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kadi maneno,<br>b) kutamka sauti lengwa ipasavyo ili kuimarisha mazungumzo,<br>c) kutamka silabi za sauti sauti lengwa ipasavyo,<br>d) kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa,<br>e) kuchangamkia nafasi ya matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kushiriki katika kutambua sauti lengwa katika kadi maneno,<br>● kusikiliza mwalimu au mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa,<br>● kutamka sauti alizozisikiliza pamoja na mwalimu na mwishowe kutamka akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia vifaa vya kidijitali (*k.v. papaya*) kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kutamka sauti lengwa ashirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na | Kwa ninini muhimu kutamka maneno ipasavyo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali k.v. kinasasauti na rununu,<br>● kutamka silabi alizozisikiliza ipasavyo akishirikiana na wenzake,<br>● kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kumwomba mzazi au mlezi kutumia kifaa cha kidijitali kama vile rununu ili kusikiliza matamshi ya sauti lengwa. | |

- **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirki kikamilifu katika shughuli za kikundi kutamka sauti, silabi na maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia teknolojia kujifunzia matamshi bora ya sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti, silabi na maneno ipasavyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>●  Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujifunza matamshi ya sauti lengwa, silabi na maneno.<br>●  Haki za kijamii: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake kutoka jamii mbalimbali.<br>●  Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamkiana na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa kwa utulivu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Uzuiaji wa magonjwa: mwanafunzi anaposoma maneno yanayohusu suala lengwa atapata fursa ya kujifunza uzuiaji wa magonjwa kwa kula chakula kifaacho. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>•  Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora na jinsi inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>•  Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti: (/j/, /r/, /p/, /f/, /v/, /sh/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 25 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi)* akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijitali, nk akishirikiana na wenzake, akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kwa sauti inayosikika, | Matamshi bora na sauti inayosikika yana umuhimu gani katika kusoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kwa sauti inayosikika. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika shughuli za kikundi kutambua silabi, maneno na sentensi zenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua silabi, maneno na sentensi zenye sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusoma kifungu cha hadithi ifaavyo.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma kwa ufasaha ili kufankisha mawasilano.

**Masuala mtambuko:**

- Matumizi yafaayo ya vitu nyumbani: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu vyakula k.v. vyakula vinavyotumiwa nyumbani.
- Upataji wa pesa: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu vyakula k.v. uuzaji wa vyakula.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya silabi katika somo hili na dhana zinazofunzwa katika masomo ya *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya  mazingira..

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Tahajia**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi tatu kuhusu suala lengwa akizingatia tahajia sahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya tahajia sahihi katika uandishi wa sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sentensi zinazohusu suala lengwa zenye tahajia sahihi kwa kutumia nyenzo kama vile: kadi za majina, mti maneno, kapu maneno, chati, kifungu au kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma sentensi zenye tahajia sahihi kuhusu suala lengwa,<br>● kunakili sentensi zenye tahajia sahihi kuhusu suala lengwa kwenye daftari,<br>● kutunga sentensi tatu sahihi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika sentensi alizotunga kwa kuzingatia tahajia sahihi,<br>● kusoma sentensi alizoandika pamoja na wenzake katika kikundi kisha wenzake wazitolee maoni,<br>● kusahihisha sentensi alizoandika kwa kuzingatia tahajia, | Kwa nini ni muhimu kuyaandika maneno na sentensi kwa usahihi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • Kumwonyesha mzazi au mlezi sentensi sahihi alizoandika ili apate maoni yake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia kikamilifu katika kikundi kutambua na kutunga sentensi kwa kuzingatia tahajia sahihi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kuandika sentensi na kumtumia mwalimu mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga na kuandika sentensi akizingatia tahajia sahihi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutunga sententensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima na umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Upendo: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kuandika sentensi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika sentensi alizotunga kwa kuzingatia tahajia sahihi.

**Masuala mtambuko:**

- Matumizi yafaayo ya vitu nyumbani: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa k.v. vyakula vinavyotumiwa nyumbani.
- Elimu ya pesa: mwanafunzi anapoandika sentensi zenye tahajia sahihi kuhusu suala lengwa k.v. uuzaji wa vyakula.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika na kuzingatia tahajia inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia hali ya mazingira.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Matumizi ya hiki na hivi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno **hiki** na **hivi** katika vifungu,<br>b) kusoma vifungu vinavyojumuisha maneno **hiki** na **hivi** ili kuonyeshea ifaavyo,<br>c) kutumia maneno **hiki** na **hivi** kuonyeshea vitu katika mazingira yake,<br>d) kuchangamkia matumizi ya **hiki** na **hivi** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua **hiki** na **hivi** kwa kutumia nyenzo halisi, kadi za majina, kapu maneno au chati,<br>● kusikiliza kifungu kinachohusu matumizi ya **hiki** na **hivi** katika kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma vifungu vinavyojumuisha **hiki** na **hivi** kisha abainishe matumizi ya **hiki** na **hivi,**<br>● kuonyesha vitu mbalimbali kama vile vyakula na kuvitungia sentensi katika kikundi k.m. *chakula hiki – vyakula hivi*,<br>● kumtungia mwenzake sentensi katika kikundi kwa kutumia **hiki** na **hivi,**<br>● kutoa maoni kuhusu sentensi zilizotungwa na wenzake,<br>● kukamilisha vifungu vyenye mapengo kwa kutumia **hiki** na **hivi** wakiwa wawiliwawili k.m. chakula _____ (hiki, hii), vyakula _____(hivi, hizi) | Unajua majina yapi ya vitu vinavyoweza kuashiriwa kwa kutumia maneno **hiki** na **hivi**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia kikamilifu katika kikundi kwa kutunga sentensi akitumia **hiki** na **hivi**.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikisha mzazi au mlezi wake kutambua vitu nyumbani na katika jamii vinavyoweza kuashiriwa kwa kutumia **hiki** na **hivi.**<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia **hiki** na **hivi** ipasavyo. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi kufanya zoezi kwa kutumia kifaa cha kidijitali na kukitunza ipasavyo.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Matumizi yafaayo ya vitu nyumbani: mwanafunzi anaposoma vifungu kuhusu vyakula k.v. vyakula vinavyotumiwa nyumbani.<br>● Elimu ya pesa: mwanafunzi anaposoma vifungu kuhusu vyakula k.v. uuzaji wa vyakula. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha vionyeshi katika sarufi kama inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana hii na somo la *Environmental Activities* linaloshughulikia mazingira. |

## 9.0 JIKONI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala lengwa ili azungumze kulihusu,<br>b) kuzungumza kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora na ishara zifaazo,<br>c) kujieleza kwa ujasiri, kasi ifaayo na sauti inayosikika,<br>d) kuchangamkia mazungumzo na matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza mazungumzo mafupi kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutazama video kuhusu mazungumzo yanayohusisha watoto,<br>● kuwasilisha mazungumzo yake kwa wenzake katika kikundi kwa kuzingatia matamshi bora na ishara zifaazo,<br>● kujieleza kwa ujasiri, kasi ifaayo na sauti inayosikika,<br>● kusikiliza mazungumzo ya wenzake na kutoa maoni.<br>● kushiriki katika mazungumzo kwa kuzingatia maagizo atakayopewa na mwalimu,<br>● kujieleza kwa ujasiri ili kufanikisha mawasiliano akiwa na mzazi au mlezi jikoni. | 1. Unapenda kuzungumza kuhusu mambo gani ukiwa na wenzako?<br>2. Unazingatia mambo gani unapozungumza mbele ya wenzako? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuwasilisha mazungumzo mbele yao.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunza mazungumzo.<br>● Uraia: mwanafunzi anapoingiliana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama video.<br>● Heshima: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika mazungumzo na kuwapa nafasi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.<br>● Elimu ya pesa: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa akielezwa na mwalimu. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya mazungumzo inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha ufahamu chenye maneno 23-30 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v. kisu, kikombe, meko, sahani)* akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa. | Je, tunaweza kujifunza mambo yapi kutokana na hadithi mbalimbali? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutambua ujumbe katika kifungu.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Uraia: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotabiri matukio ya hadithi kwa kutazama picha. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadiliana.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu darasani.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kusoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya pesa: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu shughuli za jikoni k.v. ununuzi wa vitu vya jikoni na bei yake kutokana na suala lengwa.<br>● Mshikamano ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa k.v. vifaa vya jikoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Kifungu kutokana na Picha**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutazama picha na kutambua yaliyomo,<br>b) kuandika kifungu kuhusu yaliyomo katika picha,<br>c) kufurahia kuandika kifungu kutokana na yaliyomo katika picha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama picha na kutambua wahusika, walipo wahusika na matendo yao akiwa peke,<br>● kuandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali kifungu cha sentensi mbili kutokana na picha aliyoitazama,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichokiandika ili ampe maoni yake. | Ni ujumbe upi unaoweza kuutoa kutokana na picha baada ya kuitazama? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua yaliyomo katika picha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofaulu kusoma picha na kuandika kinachoendelea katika picha hiyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali na anapoandika ifaavyo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya pesa: mwanafunzi anapotazama picha kuhusu suala lengwa.<br>● Matumizi yafaayo ya vitu nyumbani: mwanafunzi anapotazama picha na kutambua vifaa vya jikoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Matumizi ya Maneno Yanayoashiria Vitendo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze;<br>a) kutambua maneno yanayoashiria vitendo katika kifungu na mawasiliano mbalimbali,<br>b) kusoma maneno yanayoashiria vitendo ili kujenga usomaji bora,<br>c) kutumia maneno yanayoashiria vitendo katika sentensi ipasavyo,<br>d) kufurahia kutumia maneno yanayoashiria vitendo katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayoashiria vitendo katika kadi maneno, mti maneno, chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kutaja mambo aliyofanya siku hiyo kama vile, *kula, kuvaa, kupika, kuwasha, kuosha, pakua,*<br>● kuigiza vitendo k.m. *kula, kunywa, keti, simama, nawa, choma,*<br>● kusoma maneno yanayoashiria vitendo ili kujenga usomaji bora,<br>● kukamilisha sentensi akitumia maneno yanayoashiria vitendo,<br>● kutunga sentensi zenye matumizi ya maneno yanayoashiria vitendo,<br>● kumtungia mwenzake katika kikundi sentensi kwa kutumia maneno yanayoashiria vitendo,<br>● kufanya zoezi la kujaza nafasi katika madaftari yao. | Je, ni mambo yapi uliyofanya tangu jana? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika utunzi wa sentensi na wenzake katika kikundi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotungia mwenzake sentensi kwa kutumia maneno yanayoashiria vitendo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofanya zoezi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia maneno yanayoashiria vitendo. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika shughuli za kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia maneno yanayoashiria vitendo.<br>● Haki za kijamii: mwanafunzi anapoigiza vitendo akiwa na mwenzake huku akizingatia maslahi ya mwenzake k.v. ikiwa mwenzake ana mahitaji maalumu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Matumizi ya pesa: mwanafunzi anapojifunza vitendo k.v. nunua. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vitenzi inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

## 10.0 MICHEZO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Sauti: (/ny/, /dh/, /th/, /ch/, /gh/, /ng/, /ng'/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kadi maneno,<br>b) kutamka sauti lengwa ipasavyo ili kuimarisha mazungumzo,<br>c) kutamka silabi za sauti lengwa ipasavyo,<br>d) kutamka ipasavyo maneno yenye silabi za sauti lengwa,<br>e) kuchangamkia nafasi ya matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kushiriki katika kutambua sauti lengwa katika kadi maneno,<br>● kutumia teknolojia (*k.v. papaya*) kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kusikiliza mwalimu au mgeni mwalikwa akitamka sauti lengwa,<br>● kutamka sauti pamoja na mwalimu,<br>● kutamka sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua majina ya herufi zinazowakilisha sauti lengwa kwa kutumia kadi za herufi, | Ni majina yapi ya sauti */ny/,/dh/,/th/,/ch/, /gh/,/ng/, /ng'/*unayojua kutamka? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kutamka herufi za sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali k.v. kinasasauti na rununu,<br>• kutamka silabi alizozisikiliza ipasavyo akishirikiana na wenzake,<br>• kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ipasavyo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutamka sauti na maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia teknolojia kujifunzia matamshi bora ya sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka sauti na silabi ipasavyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamkiana na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa.<br>● Haki za kijamii: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake kutoka jamii mbalimbali. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya kazi ya kikundi.<br>● Masuala ya afya: mwanafunzi anapotumia maneno yanayohusu suala lengwa.<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anapojifunza kutokana na suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora na yale yanayofunzwa katika masomo ya *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la michezo na somo la *Creative Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Ufasaha:**<br><br>*Sauti: (/ny/, /dh/, /th/, /ch/, /gh/, /ng/, /ng'/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kiwango kifaacho cha sauti,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye suala lengwa (k.m kuhusu michezo mbalimbali, sehemu mbalimbali za barabara kwa kuzingatia kasi ifaayo **(*m****aneno 30 kwa dakika na kwa kizingatia viakifishi*) akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k akishirikiana na wenzake kwa kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti, | Je, tunafaa kufanya nini tunapowasomea wengine kitabu kwa sauti? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na kiwango kifaacho cha sauti. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposoma silabi, maneno na sentensi zenye sauti lengwa pamoja na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia teknolojia kujifunzia.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kusoma maneno na sentensi zenye sauti lengwa ipasavyo.

**Maadili:**

- Haki za kijamii: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake kutoka jamii mbalimbali.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutamka na kurekebishana matamshi ya sauti lengwa kwa utulivu.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya maendeleo endelevu: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma na yale yanayofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la michezo na somo la *Creative Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali dadisi lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Kifungu kutokana na picha**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutazama picha na kutambua yaliyomo,<br>b) kuandika kifungu kuhusu yaliyomo katika picha,<br>c) kufurahia kuandika kifungu kutokana na yaliyomo katika picha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama picha kuhusu suala lengwa na kutambua wahusika na matendo yao akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza wenzake katika kikundi wahusika ni nani na wanafanya nini,<br>● kuandika kifungu cha sentensi mbili kutokana na picha aliyoitazama,<br>● kuwasomea wenzake sentensi alizoandika kuhusu picha,<br>● kunakili sentensi alizoandika kwa kutumia kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika kifungu kwa kurejelea baadhi ya picha zinazopatikana nyumbani na sehemu mbalimbali za barabarani. | Unapenda picha zinazohusu vitu gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu katika kueleza yaliyomo katika picha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikisha mzazi au mlezi kuandika kifungu kwa kurejelea baadhi ya picha zinazopatikana nyumbani.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wanapofanya shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Kujithamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu kutokana na picha. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika kama inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la michezo na somo la *Creative Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vitendo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo mbalimbali katika kifungu chepesi,<br>b) kutumia majina ya vinyume vya vitendo katika mawasiliano,<br>c) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma maneno ya vitendo na vinyume vyake akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua vinyume vya vitendo (*kama vile, lala-amka; keti - simama; cheka - lia; enda - rudi; panda*- *shuka*) katika kadi maneno, mti maneno, chati, kapu maneno au vifaa vya kidijitali<br>● kutumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo k.v. katika kifungu kinachosomwa,<br>● kuigiza vinyume vya vitendo akiwa katika kikundi,<br>● kushirikishwa kutaja majina ya vinyume vya vitendo,<br>● kuandika vinyume vya vitendo. | Je,vinyume gani vya vitendo unavyofanya kila siku? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawisiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza vinyume vya vitendo katika kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya teknolojia kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya vinyume vya vitendo mbalimbali. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Kujitambua: mwanafunzi anapoigiza vinyume vya vitendo mbele ya wenzake. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume vya maneno na kama inavyofunzwa katika masomo ya *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la michezo na somo la *Creative Activities.* |

## MWONGOZO WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA

## MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutumia ishara za mwili ipasavyo katika mawasiliano.** *(kuketi, kusimama na ishara za uso)* | Anatumia ishara za mwili ipasavyo katika mawasiliano kila wakati. | Anatumia ishara za mwili ipasavyo. | Anatumia baadhi ya ishara za mwili ipasavyo. | Anatumia baadhi ya ishara za mwili kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa.** (*matamshi ya sauti zinazokaribiana:* Sauti za /n/, /f/, /v/, /o/, /ch/, /*ny*/, /*ng*/, /sh/, /th/, /w/, /e/, /i/, /h/, /s/, /b/, /y/, /z/, /g/, /d/, /j/, /r/, /p/, /m/, /a/, /u/, /k/, /t/, /th/, /gh/, /dh/ alfabeti ya Kiswahili. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa kila wakati. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa kwa kuelekezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** *(Matamshi, kasi ifaayo na kusikika)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo na sauti inayosikika katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha kwa akizingatia matamshi, kasi ifaayo na sauti inayosikika. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha kwa kuzingatia baadhi ya matamshi bora, pasipo kuzingatia kasi ifaayo na sauti inayosikika. | Anazungumza na kujieleza kwa kuzingatia baadhi ya matamshi bora, pasipo kuzingatia kasi ifaayo na sauti inayosikika kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo (***msamiati wa heshima, adabu, maamkuzi, maagano na maagizo.)* | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano, kutumia msamiati wa heshima na adabu kwa urahisi. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano, kutumia msamiati wa heshima na adabu. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano, kutumia baadhi ya msamiati wa heshima na adabu. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano, kutumia baadhi ya msamiati wa heshima na adabu kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutoa ujumbe katika hadithi aliyoitoa kikamilifu.** *(msamiati, ujumbe katika hadithi)* | Anatoa ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu na kwa utendeti. | Anatoa ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu. | Anatoa baadhi ya ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu.. | Anatoa baadhi ya ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu kwa kusaidiwa. |

**MADA: KUSOMA**

| Viwango<br>Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kusoma**.<br>(*kushika kitabu na kuelekeza macho kutoka kushoto hadi kulia)* | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kusoma kwa uketo. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kusoma. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kusoma. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kusoma kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu - Vifungu.**<br>*( ujumbe, msamiati)* | Anasoma vifungu, kutambua ujumbe na matumizi mwafaka ya msamiati kila wakati. | Anasoma vifungu, kutambua ujumbe na matumizi mwafaka ya msamiati. | Anasoma vifungu, kutambua baadhi ya ujumbe na baadhi ya matumizi mwafaka ya msamiati. | Anasoma vifungu, kutambua baadhi ya ujumbe na baadhi ya matumizi mwafaka ya msamiati kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.**<br>(*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo akizingatia sauti lengwa.*)<br>*(/m/, /a/, /u/, /k/, /t/, /l/, /n/, /o/, /w/, /e/, /i/, /h/, /s/, /b/, /y/, /z/, /g/, /d/, /ch/, /ny/, /sh/, /th/, /ng'/, /ng/, /gh/, /th/)* | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa kuelekezwa. |

**MADA: KUANDIKA**

| Viwango / Vigezo | Kuzidi matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kuandika**. *(kuketi wima, kushika kalamu, ipasavyo, kuandika kutoka kushoto hadi kulia)* | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kuandika kila wakati. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kuandika. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kuandika. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kuandika kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuandika kwa hati nzuri sentensi na kifungu kifupi kwa kuzingatia tahajia na hati nadhifu.** *(herufi ndogo, herufi kubwa ,kifungu kutokana na picha na imla)* | dika kwa hati nadhifu kwa kuzingatia tahajia kila wakati. | Anaandika kwa hati nadhifu kwa kuzingatia tahajia. | Anaandika kwa hati isiyo nadhifu kwa kutozingatia baadhi ya tahajia. | Anaandika kwa hati isiyo nadhifu kwa kutozingatia baadhi ya tahajia kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuzingatia muundo na mtindo wa kuandika na kuhariri sentensi au matini** (uakifishaji ufaao*)* | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu kila wakati. | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu. | Anazingatia baadhi ya vipengele vya muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu. | Anazingatia baadhi ya vipengele vya muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu kwa kusaidiwa |

**MADA: SARUFI**

| Viwango<br>Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia maneno mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.** **(***mimi na sisi , huyu na hawa,  -angu na etu,hiki na hivi, -zuri na –baya )* | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini kwa ufasaha. | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika lugha ya kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika matini kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno.** *(Vinyume vya vitenzi)* | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno kwa utendeti. | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno kwa kusaidiwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia umoja na wingi wa majina, maneno yanayoashiria vitendo**(*umoja, wingi na vitenzi)* | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa majina na maneno yanayoashiria vitendo kwa utendeti. | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa majina na maneno yanayoashiria vitendo. | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa baadhi majina na maneno yanayoashiria vitendo. | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa baadhi ya majina na meneno yanayoashiria vitendo kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua ukanusho wa nafsi ya kwanza umoja na wingi.** *( ukanushaji wa nafsi ya kwanza)* | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya kwanza umoja na wingi kwa kina. | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya kwanza umoja na wingi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya kwanza umoja na wingi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya kwanza umoja na wingi kwa kusaidiwa. |

# KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA
# GREDI YA 2

## 1.0 SHULENI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano ya nyakati za siku,<br>b) kuamkua na kuitikia maamkuzi na maagano ya nyakati za siku,<br>c) kufurahia kuamkua na kuagana ili kujenga mshikamano wa kijamii. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi mbalimbali ya nyakati za siku (*habari ya asubuhi*, *habari ya mchana*, *Habari ya jioni*, *siku njema*) kutoka kwenye chati, vitabu, kadi maneno, mti maneno, michoro, picha au vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kutazama picha za watu wakisalimiana na kuagana akishirikiana na wenzake kujadili picha hizo,<br>• kutazama video inayoonyesha watu wakitumia maamkuzi na maagano ya nyakati za siku,<br>• kuigiza na mwenzake maamkuzi na maagano mbalimbali. | Tunaamkuana vipi wakati wa asubuhi, mchana na jioni? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika kazi ya kikundi na kujadiliana kuhusu maamkuzi na maagano ya nyakati za siku.

| |
|---|
| • Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama watu wakisalimiana na kuagana.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza ipasavyo maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili picha za watu wanaoamkuana na kuagana. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaamkua wengine kwa heshima.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowaamkua na kuwaaga wenzake.<br>● Amani: mwanafunzi anapowaamkua na kuwaaga wenzake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapojumuika na wenzake katika kuigiza maamkuzi na maagano darasani, shuleni na katika mazingira yake. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maamkuzi na maagano aliyojifunza katika somo la Kiwahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma Ufahamu**<br>*Kusoma kifungu.*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 31 - 34 na kutambua msamiati wa suala lengwa akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa. | Kusoma kifungu ili ufahamu ujumbe unafanya nini? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuchangia katika kutambua msamiati, kutabiri na kujibu maswali.<br>• Uwazaji wa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa utabiri kutokana na picha na kuchangia katika kujibu maswali.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kijiditali kusoma hadithi na kutazama picha. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi kujadiliana.<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapoeleza mafunzo kutokana na kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma hadithi na pia kujadili picha ukakamavu wake unaimarika.<br>● Utunzaji na matumizi yafaayo ya vitu vinavyopatikana shuleni: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufahamu na aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Hati nadhifu:**<br><br>**Sentensi:** *Maumbo yanayofaa, kutoacha nafasi baina ya herufi katika neno, kuacha nafasi kati ya neno lingine*),<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua hati nadhifu katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi akizingatia hati nadhifu,<br>c) kufurahia kuandika akizingatia hati nadhifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua hati nadhifu kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>• kujadili na wenzake kuhusu hati nadhifu kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali,<br>• kuandika sentensi fupi kuhusu suala lengwa akizingatia hati nadhifu,<br>• kuwasilisha darasani sentensi zake ili wenzake wamtolee maoni,<br>• kumwandikia mzazi au mlezi sentensi fupi kuhusu suala lengwa akizingatia hati nadhifu. | Je, ni mambo gani unayozingatia wakati wa kuandika? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu hati nadhifu. Pia, anaposhiriki kikamilifu kuandika akiwa na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotambua hati nadhifu katika kifaa cha kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoandika akizingatia hati nadhifu.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli ya kuandika.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu hati nadhifu uwezo wake wa uandishi bora unakuzwa.<br>• Usalama mtandaoni: mwanafunzi azingatie hatua za kiusalama anapotambua hati nadhifu kwenye kifaa cha kidijitali. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kuandika kwa hati nadhifu anayojifunza katika somo hili na ujifunzaji<br>wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Matumizi ya Wewe na Nyinyi**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua **wewe** na **nyinyi** katika sentensi,<br>b) kutumia **wewe** na **nyinyi** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kufurahia kutumia **wewe** na **nyinyi** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusikiliza kifungu au wimbo unaohusu nafsi ya pili (**wewe** na **nyinyi**), kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali,<br>• kusoma vifungu vilivyo na nafsi ya pili (**wewe** na **nyinyi**) akishirikiana na wenzake,<br>• kutumia nafsi ya pili (**wewe** na **nyinyi**) umoja na wingi kwa kuigiza mazungumzo na wenzake katika kikundi (*k.m: Wewe unasoma - Nyinyi mnasoma; Wewe ulienda shuleni - Nyinyi mlienda shuleni.),*<br>• kujaza nafasi kwa kutumia wewe na **nyinyi,**<br>• kutaja zoezi la nafsi ya pili kwenye tarakilishi kwa kuburura majibu sahihi na kujaza nafasi akielekezwa na mwalimu,<br>• kuwasiliana na mzazi au mlezi wake kwa kutumia nafsi ya pili **(wewe** na **nyinyi)**. | Ni neno gani unaloweza kutumia kuwataja wenzako bila kutaja majina yao? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kutoa mifano kwa kutumia **wewe** na **nyinyi.**
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **wewe** na **nyinyi**.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya **wewe** na **nyinyi.**
- Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia wewe na **nyinyi** ifaavyo.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anashirikiana na wenzake katika kuigiza matumizi ya wewe na mimi na kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake na kuwapatia nafasi kushiriki katika majadiliano.
- Upendo: mwanafunzi anapokuwa tayari kushirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kuigiza mazungumzo ya nafsi ya pili **wewe** na **nyinyi.**

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya wewe na nyinyi aliyojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.*

## 2.0 HAKI ZANGU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Matamshi Bora.**<br><br>*Sauti: /p/, /f/, /v/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maandishi,<br>b) kutamka ipasavyo silabi za sauti lengwa katika maandishi,<br>c) kutamka maneno mepesi yanayotokana na sauti lengwa katika maandishi,<br>d) kusoma ipasavyo sentensi nyepesi zenye sauti lengwa kwa matamshi bora,<br>e) kuchangamkia usomaji bora wa maneno yanayotumia sauti | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi kwenye maneno yenye sauti lengwa katika sentensi akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza silabi lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka silabi za sauti lengwa akiwa peke yake au na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno yenye sauti lengwa yaliyotamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali akiwa peke yake, au na wenzake akizingatia matamshi bora,<br>● kusikiliza sentensi zenye sauti lengwa zikisomwa na mwalimu, | Je, kwa nini ni vizuri kutamka maneno vizuri tunapozungumza? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>lengwa katika mawasiliano.</td><td>mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma sentensi za sauti lengwa zilizosomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake kwa kuzingatia matamshi bora,<br>● kujirekodi kwa kutumia kifaa cha kidijitali akitamka sentensi za sauti lengwa na kuwatumia wenzake ili watazithmini,<br>● kukariri mashairi na nyimbo katika tamasha za mziki au kwenye hafla shuleni ili kuboresha matamshi kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>● kuwasiliana na mzazi au mlezi wake kwa kutumia maneno yenye sauti lengwa.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma sentensi na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotamka sauti lengwa ipasavyo darasani.</td></tr>
</table>

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka sauti lengwa katika sentensi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi na kuwakosoa kwa heshima. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujirekodi na kutumia wenzake azingatie hatua za kiusalama.<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake darasani kutamka sauti lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora, stadi anayojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa ufasaha.**<br><br>*Sauti: /p/, /f/, /v/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yenye sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yenye sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kuhusu haki za mtoto (*k.v. upendo, mavazi, makao, chakula*) kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 33 kwa dakika)* na kwa kuzingatia viakifishi,<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali akiwa peke yake, au na wenzake, akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zinazofaa, | Je, ni mambo gani unayozingatia ili kusoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutambua sauti na kusoma maneno na sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma maneno na sentensi zenye sauti lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kutoa mchango wao.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na kushirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua majukumu mbalimbali katika kazi ya kikundi.

**Masuala mtambuko:**

- Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu haki za watoto akizingatia matamshi bora, kasi ifaayo, sauti inayosikika na ishara zifaazo.
- Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma kifungu kinachuzungumzia suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma anayojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati Nadhifu**<br>*Herufi Kubwa*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mpangilio ufaao wa herufi kubwa katika matini,<br>b) kuandika herufi kubwa ipasavyo katika maneno na sentensi,<br>c) kufurahia kutumia herufi kubwa ipasavyo katika maneno na sentensi ili kuboresha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mpangilio ufaao wa herufi kubwa katika matini *(k.v. kadi maneno, mti maneno, picha, chati, kitabu, kifaa cha kidijitali, n.k.)* akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kunakili maneno na sentensi kuhusu mada lengwa *(k.v upendo, kupata elimu, chakula, mavazi, makazi)* kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kutunga na kuandika sentensi fupi akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kushirikiana na wenzake kutathmini sentensi walizotunga,<br>● kumwandikia mzazi au mlezi maneno kwa kutumia mpangilio ufaao wa herufi kubwa na hati nadhifu. | Je herufi kubwa huwa na sifa gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapofaulu kuwaonyesha wenzake herufi kubwa ilipotumiwa katika maneno na sentensi. Pia anaposhiriki kutambua na kuandika herufi kubwa katika kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika herufi kubwa katika maneno na sentensi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwandikia mlezi au mzazi wake maneno kwa kutumia herufi kubwa ipasavyo. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaponakili maneno na sentensi kuhusu haki za watoto kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa herufi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya herufi kubwa katika somo hili na anayojifunza katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Vifungu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi,<br>b) kuandika vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia vifungu vya maneno katika umoja na wingi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi katika matini mbalimbali, kadi maneno, mti maneno, vifaa vya kidijitali,<br>• kuandika vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake. (*k.v chakula changu-vyakula vyetu)*<br>• kujaza nafasi kwa kukamilisha vifungu vya maneno katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>• kushiriki katika mchezo wa kupanga kadi za vifungu vya maneno akiambatanisha umoja na wingi,<br>• kumwonyesha mzazi au mlezi wake vifungu vya maneno alivyoviandika kwa umoja na wingi. | Umoja na wingi wa vifungu huwa na sifa gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika vifungu vya maneno.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika vifungu vya maneno katika umoja na wingi. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika vifungu vya maneno katika umoja na wingi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali ipasavyo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kuandika vifungu vya maneno mawili katika umoja na wingi.<br>• Haki za watoto: mwanafunzi anaposhiriki kuandika sentensi kuhusu haki za watoto. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya umoja na wingi katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.* . |

## 3.0 LISHE BORA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Heshima na Adabu**<br><br>*Hodi, karibu, tafadhali, ninaomba, nisamehe na nashukuru.*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu yanayotumiwa katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano akiambatanisha na hisia zifaazo,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua maneno ya heshima na adabu yanayotumiwa katika jamii,<br>• kujadili ni lini maneno husika yanatumiwa katika mawasiliano akiwa na wenzake,<br>• kutazama michoro mbalimbali na kujadili neno linalofaa kutumiwa katika miktadha husika,<br>• kutazama video kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu, | Maneno ya adabu huwa na sifa gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuambatanisha matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mazungumzo na hisia katika maigizo,<br>• kuwasiliana na mzazi au mlezi kwa kutumia maneno ya adabu na heshima ifaavyo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika majadiliano kuhusu maneno ya heshima na adabu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama maigizo kuhusu vitendo vya heshima na adabu.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili matumizi ya maneno ya heshima na adabu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya heshima na adabu.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kutoa hoja zao katika kikundi na pia anapotumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano.<br>• Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotazama video kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu azingatie hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala hili la lishe bora na masuala yanayofunzwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br>*Kusoma kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 35 -38 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(afya*, *nguvu*, *protini*, *wanga*, *vitamini)* akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu cha hadithi kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake, | Je unazingatia nini ilikupata ujumbe katika ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kuchangia kikamilifu katika kueleza ujumbe wa kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali kutazama picha na kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake na kumweleza ujumbe katika kifungu chepesi.
- Uwazaji kwa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotabiri na kufikia uamuzi wa mafunzo anayopata kwenye kifungu cha ufahamu.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi kujadili ujumbe na kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia kujifunzia.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha hadithi na kutumia msamiati kuhusu lishe bora, ujuzi wake wa kujikinga dhidi ya maradhi mbalimbali unapanuka.
- Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa kuhusu lishe bora.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu na katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.*

Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala hili la lishe bora na masuala yanayofunzwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Mpangilio wa Herufi Ndogo**<br><br>(Vipindi 3) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mpangilio ufaao wa herufi ndogo katika maandishi,<br>b) kuandika kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo,<br>c) kuchangamkia kuandika vifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mpangilio ufaao wa herufi ndogo katika maandishi kwenye kadi maneno, chati, daftari au kifaa cha kidijitali,<br>● kuwaonyesha wenzake mpangilio ufaao wa herufi ndogo kwenye kadi maneno, kitabu, chati au kifaa cha kidijitali,<br>● kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo akishirikiana na wenzake,<br>● kutumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo,<br>● kutunga kifungu kuhusu suala lengwa akizingatia mpangilio unaofaa. | Kwa nini ni vizuri kuandika herufi ndogo ipasavyo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kuandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha maneno akitumia kifaa cha kidijitali.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufu ndogo. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuthamini maoni ya wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake kutoka jamii mbalimbali wanaposhirikiana kunakili kifungu wakizingatia mpangilio ufaao wa herufi ndogo. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya herufi ndogo katika uandishi katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala hili la lishe bora na masuala yanayofunzwa katika somo la Environmental Activities |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Matumizi ya Huyo na Hao**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **huyo** na **hao** katika kifungu,<br>b) kutumia **huyo** na **hao** katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **huyo** na **hao** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **huyo** na **hao** kwa kutumia nyenzo kama vile kadi maneno, mti maneno, kapu maneno au chati,<br>● kusilikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya **huyo** na **hao** katika kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua **huyo** na **hao** katika kifungu au wimbo aliosikiliza kwa kuongozwa na mwalimu,<br>● kusoma sentensi zenye kudhihirisha matumizi ya **huyo** na **hao** kama vile:<br>*mtoto **huyo** anakula chakula.*<br>*Watoto **hao** wanakula chakula.* | Ni maneno gani yatatumiwa kuonyesha mwenzako akiwa mbali kidogo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia huyo na hao,<br>• kumtungia mwenzake katika kikundi sentensi kwa kutumia **huyu** na **hao,**<br>• kuandika sentensi zinazodhihirisha matumizi ya **huyo** na **hao** kama vile: *mtoto* ***huyo*** *anasoma* *watoto* ***hao*** *wanasoma*<br>• kujaza nafasi kwa kutumia **huyo** na **hao** akielekezwa na mwalimu. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia **huyo** na **hao**.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **huyo** na **hao** akishirikiana na wenzake katika kikundi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia huyo na **hao** kwa lugha fasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kurejelea watu wa familia yake kwa kutumia **huyo** na **hao** ipasavyo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **huyo** na **hao.**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kumshirikisha mzazi au mlezi wake katika kurejelea watu wa familia yake kwa kutumia maneno **huyu** na **hao**. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu wenye upungufu wa lishe bora kwa kutumia **huyo** na **hao.** |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya vivumishi vya nafsi katika somo hili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activitie na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala hili la lishe bora na masuala yanayofunzwa katika somo la *Environmental Activities.* |

## 4.0 USAFIRI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora** *Sauti; /ch/ na /dh/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa akizingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa *(/ch/* na */dh/*) katika maneno kwenye kadi maneno, chati, mti maneno, sentensi, au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kushirikiana na kutumia kifaa cha kidijitali *(k.v. kupitia Programu ya Papaya)* kusikiliza matamshi bora ya silabi za sauti lengwa,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakisomwa na wenzake darasani kisha kutambua sauti hizo katika maneno hayo,<br>● kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ifaavyo akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya silabi za sauti lengwa kutoka kwa kitabu au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake, | Je, ni maneno gani unayojua yenye sauti /ch/ na /dh/? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kuimba wimbo akizingatia sauti lengwa kuhusu kuweka mazingira ya barabara safi. . | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali akisoma kifungu na kutamka sauti lengwa ipasavyo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutamka sauti lengwa ipasavyo.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana katika vikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za vikundi.

**Masuala mtambuko:**

Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa azingatie hatua za kiusalama.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafiri na suala la *Evironmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa ufasaha**<br>*Sauti; /ch/, /dh/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika matini mbalimbali,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kufurahia kusoma kifungu ipasvyo ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti /*ch*/na /*dh*/ katika kadi maneno, mti maneno au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno au hadithi yenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno au hadithi yenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, sauti inayosikika akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno au hadithi yenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, kasi ifaayo (maneno 36 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi) akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k akishirikiana na wenzake na kuzingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo, | Je, ni mambo gani unazingatia kusoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k akishirikiana na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia matamshi ya sauti lengwa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoendelea kusoma vifungu mbalimbali maishani.

**Maadili**:

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi wakati wa shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika kikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposoma kifungu chepesi kwa kutumia ishara zifaazo.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kusoma kifungu cha hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijaitali.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English *Language Activities na Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafiri na suala la *Evironmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Nafasi katika maandishi.**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi kati ya maneno katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno katika sentensi kwa maandishi,<br>c) kufurahia kuandika akizingatia nafasi kati ya maneno katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua nafasi kati ya maneno katika sentensi akishirikiana na wenzake,<br>• kuwaonyesha wenzake nafasi kati ya maneno katika sentensi akishirikiana na wenzake, kuandika sentensi kuhusu suala lengwa akizingatia nafasi kati ya maneno,<br>• kuwasomea wenzake sentensi alizoziandika kuhusu usafiri na usalama barabarani ili wazitolee maoni,<br>• kutumia kifaa cha kidijitali kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno. | Je, kwa nini tunatumia nafasi kati ya maneno katika sentensi? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuonyesha nafasi kati ya maneno katika sentensi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno kwa kutumia kifaa cha kidijitali.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya mazoezi ya ziada ya kuandika sentensi akizingatia nafasi kati ya maneno. | | | | |

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Usalama wa watoto barabarani: mwanafunzi anapotunga sentensi sahili zinazohusu mada lengwa ya usafiri hasa usalama barabarani.<br>• Masuala ya fedha: mwanafunzi anapoandika vifungu kuusu matumizi ya fedha katika usafiri. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafiri na suala la *Evironmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na Wingi:**<br><br>*Vifungu vya maneno*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi,<br>b) kusoma vifungu vya maneno katika umoja na wingi,<br>c) kuandika umoja na wingi wa vifungu vya maneno,<br>d) kuchangamkia kutumia vifungu vya maneno katika umoja na wingi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi (*k.m basi hili - mabasi haya; safari hii - safari hizi; ndege hii - ndege hizi; baiskeli yangu - baiskeli zetu),*<br>• kusoma vifungu vya maneno katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake, kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali akizingatia usafiri,<br>• kuandika umoja na wingi wa vifungu vya maneno akishirikiana na wenzake,<br>• kujaza nafasi zilizo wazi ili kukamilisha vifungu vya maneno katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake, | Je, unapozungumzia umoja na wingi wa maneno au sentensi unamaanisha nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kushiriki katika mchezo wa kupanga kadi za vifungu vya maneno akiambatanisha umoja na wingi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kuandika vifungu vya maneno akiwa na wenzake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoeleza kuhusu vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua vifungu vya maneno katika umoja na wingi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuheshimu maoni yao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko:**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma kifungu na kutambua maneno ya umoja na wingi kuhusu suala lengwa kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.
- Usalama wa watoto barabarani: wanapotunga sentensi kuhusu suala lengwa la usafiri.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha sarufi inayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafiri na suala la *Evironmental Activities.*

## 5.0 MNYAMA NIMPENDAYE

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1** *Ufahamu wa Kusikiliza Hadithi* **(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua picha kuhusu suala lengwa,<br>b) kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika hadithi aliyoisikiliza,<br>c) kujibu maswali kuhusu hadithi aliyoisikiliza,<br>d) kueleza ujumbe wa hadithi aliyoisikiliza,<br>e) kufurahia ufahamu wa kusikiliza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua picha kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kujadili picha kutoka kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kutabiri kitakachotokea kwenye hadithi,<br>• kusikiliza ufahamu kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vyombo vya kidijitali,<br>• kutambua msamiati uliotumika katika ufahamu aliousikiliza akishirikiana na wenzake,<br>• kujibu maswali yanayohusiana na ufahamu aliousikiliza,<br>• kueleza maudhui ya ufahamu aliousikiliza akishirikiana na wenzake, | Kusikiliza hadithi kwa makini kuna umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsimulia mzazi au mlezi wake hadithi aliyoisikiliza kuhusu suala lengwa naye mzazi kumtolea maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua picha na kujadili ujumbe katika kifungu cha ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kujifunzia.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotabiri yatakayotokea katika hadithi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu darasani.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapomsimulia mzazi au mlezi hadithi aliyoisikiliza kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposikiliza na kusikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mnyama nimpendaye na suala la *Evironmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma Kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno 39-42 na kutambua msamiati wa suala lengwa (*kondoo, mbuzi, ng'ombe,*) akishirikiana na wenzake,<br>• kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>• kutabiri ujumbe wa kifungu cha hadithi kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake,<br>• kueleza mafunzo yanyotokana na kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>• kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma.<br>• kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano. | Je, ni mambo gani yanayokusaidia kupata ujumbe kwenye vifungu vya ufahamu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomshirikisha mzazi au mlezi kusoma na kujadili ujumbe katika kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhiriki katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapowajibikia majukumu aliyopewa katika kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya utunzaji wanyama: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi na kutambua msamiati kuhusu usalama wa wanyama.<br>● Umasikini: mwanafunzi anaposoma vifungu vinavyozungumzia kuhusu suala lengwa la mnyama nimpendaye. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mnyama nimpendaye na suala la *Evironmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Uakifishi:**<br><br>*Matumizi ya Kiulizi*<br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kiulizi katika maandishi,<br>b) kuandika kiulizi ipasavyo akizingatia umbo lake,<br>c) kutumia kiulizi ipasavyo katika sentensi,<br>d) kufurahia kutumia kiulizi katika maandishi ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua kiulizi katika maandishi kitabuni, kwenye kadi maneno, mti maneno na kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kuandika kiulizi ipasavyo akizingatia umbo lake,<br>• kutumia kiulizi ipasavyo katika sentensi,<br>• kutazama matumizi ya kiulizi kwenye vifaa vya kidijitali,<br>• kuandika kiulizi akitumia kifaa cha kidijitali,<br>• kuandika sentensi sahili akitumia kiulizi ipasavyo,<br>• kumwonyesha mzazi au mlezi sentensi zenye matumizi yafaayo ya kiulizi alizotunga ili ampe maoni yake . | Je, alama ya kiulizi hutumika vipi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowaeleza na kuwaonyesha wenzake kiulizi kilipotumiwa katika maneno na sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kiulizi katika sentensi akitumia kifaa cha kidijitali.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotamani kuendelea kuandika kiulizi ipasavyo.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.
- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wanaposhiriki katika shughuli ya kuandika.

**Masuala mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapowathamini wenzake kutoka jamii mbalimbali wanaposhirikiana kutambua na kutumia kiulizi ipasavyo.
- Usalama wa wanyama: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu usalama wa mnyama nimpendaye.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matumizi ya kiulizi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mnyama nimpendaye na suala la *Evironmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Matumizi ya -ako na –enu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi yafaayo ya -**ako** na -**enu** katika kifungu,<br>b) kutumia -**ako** na **- enu** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kuthamini matumizi ya **-ako** na **-enu** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusilikiliza kifungu au wimbo unaohusu matumizi ya –**ako** na –**enu** katika kifaa cha kidijitali,<br>• kutambua matumizi ya **-ako** na **-enu** katika kadi za maneno, mti maneno, kapu maneno na vifaa halisi kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>• kumtungia mwenzake sentensi zenye matumizi ya **-ako** na **–enu,**<br>• kusikiliza sentensi zinazotungwa na wenzake zenye matumizi ya **-ako** na **-enu** na kuzitolea maoni,<br>• kuwasilisha sentensi zenye kutumia maneno **-ako** na **–enu,**<br>• kuandika sentensi zenye **-ako** na **–enu,**<br>• kujaza nafasi kwa kutumia **-ako** na **-enu** kwa kusaidiwa na mwalimu. | Je,-**ako** na **-enu** hutumiwa wakati gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia –**ako** na **-enu.**
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutumia -**ako** na -**enu** akishirikiana na wenzake katika kikundi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia **-ako** na **-enu** kwa lugha fasaha.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kumtungia mwenzake sentensi akitumia –**ako** na **-enu.** |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka maeneo tofauti tofauti kutunga sentensi zenye matumizi yafaayo ya **-ako** na **–enu** akizingatia mada lengwa.<br>• Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu mnyama nimpendaye. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya -ako na -enu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mnyama nimpendaye na suala la *Evironmental Activities.* |

## 6.0 UKOO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora:**<br><br>*Sauti:/ny/ na /ng/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa ipasavyo katika maneno na sentensi,<br>b) kutamka maneno na sentensi zenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/ny/* na */ng/*) katika matini mbalimbali kama vile kadi za maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali akizingatia suala lengwa,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza pamoja na mwalimu, kisha kuyatamka akishirikiana na mwenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kuambatanisha silabi ili kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au | Je, unajua kutamka maneno yapi yenye sauti */ny/* na */ng/*? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kutoka kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa kuhusu suala lengwa,<br>● kujirekodi akisoma sentensi zilizo na maneno yenye sauti lengwa, akishirikiana na wenzake ajisikilize ili kutathmini matamshi bora,<br>● kushiriki katika tamasha za mashairi na nyimbo au hafla shuleni ili aimarishe matamshi yake kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>● kutumia maneno ya silabi za sauti lengwa kuwasiliana na mzazi au mlezi wake. | |
| **Umilisi wa Kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma sentensi na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapotamka sauti lengwa ipasavyo na anapojirekodi. | | | | |

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika vikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za vikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika tamasha za muziki zenye asili ya jamii mbalimbali anakuza matamshi bora na talanta yake.<br>• Haki za kijamii: mwanafunzi anaposoma maneno yanayolenga suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti: /ny/ na /ng/*<br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 39 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi)* akishirikiana na wenzake, | Je, unajua maneno yapi yaliyo na silabi za sauti */ny*/,na /*ng*/? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali akishirikirikiana wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo kuhusu suala lengwa,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu kwa ufasaha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake kwenye kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusoma darasani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kusoma kifungu chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa akizingtia matamshi bora, kasi ifaayo, sauti inayosikika na ishara zifaazo.<br>● Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa la ukoo. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language Activities. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Tahajia Imla**<br><br>*Sauti: /ny/ na /ng/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye maandishi kwa kuzingatia sauti lengwa,<br>b) kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa,<br>c) kuandika sentensi sahili kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa,<br>d) kufurahia kuandika ipasavyo maneno na sentensi kutokana na imla. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye maandishi akizingatia sauti lengwa,<br>● kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu kitabuni au katika kifaa cha kidijitali akizingatia sauti lengwa,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika maneno mepesi ya silabi tatu akizingatia sauti lengwa na suala lengwa,<br>● kushiriki mchezo wa kuandika maneno na sentensi za imla na wenzake,<br>● kuwasilishia wenzake maneno ya imla ili kuyaandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika maneno atakayosomewa na wenzake daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali, | Je, kwa nini tunahitaji kusikiliza kwa makini tunaposomewa maneno ya kuandika? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>● kuandika daftarini sentensi sahili walizotunga na kumpa mwenzake ili azitolee maoni, kisha mwalimu azisahihishe,</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa mimsingi unaokuzwa:<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapofaulu kuwwasilishia wenzake maneno mepesi ya imla na kuyaandika.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika imla akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Kujiamini: anapotunga sentensi sahili na kuziandika katika daftari ili zisahihishwe na wenzake, pamoja na mwalimu</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>● Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapotangamana na wenzake darasani katika kuandika maneno na sentensi za imla kuhusu ukoo.<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu ukoo na masuala kuhusu watoto.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika imla anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language Activities.</td></tr>
</table>

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya -refu, - kubwa, - tamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-refu, -kubwa na -tamu** katika sentensi<br>b) kutumia-**refu, -kubwa na-tamu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia-**refu, -kubwa na - tamu** – katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **-refu, -kubwa, -tamu** kwa kurejelea vitu katika mazingira yake kutoka kwa kitabu, au vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusikiliza matumizi ya-**refu**, **-kubwa, -tamu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa, wenzake na kwa kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma sentensi zinazotumia maneno-**refu, -kubwa, -tamu** zinazolenga suala lengwa,<br>● kutumia -**refu, -kubwa, -tamu** akiwa na wenzake katika kikundi kurejelea vitu katika mazingira yake kuhusu suala lengwa,<br>● kukamilisha sentensi zenye matumizi ya-**refu, -kubwa, - tamu,**<br>● kujaza nafasi zilizo wazi kwa kutumia -**refu**, **-kubwa na - tamu** katika sentensi kuhusu suala lengwa, | Je, ni maneno kama gani unayoweza kutumia kuelezea sifa za kitu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuwasiliana na mlezi au mzazi kwa kutumia-**refu , - kubwa na -tamu** kuelezea vifaa kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia -**refu, -kubwa, -tamu** akiwa na wenzake katika kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza matumizi ya-**refu, - kubwa, na - tamu**.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotumia -**refu, -kubwa, -tamu** akiwa na mzazi au mlezi nyumbani.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia -**refu, -kubwa,** na**-tamu**.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.
- Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya vikundi.

**Masuala mtambuko:**

- Utangamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi akishirikiana na wenzake akizingatia mazingira ya nyumbani.
- Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapotunga sentensi zinazolenga suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kutumia lugha usahihi kisarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

## 7.0 SEBULENI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo**<br><br>*Maagizo ya hatua mbili.*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi ya hatua mbili yanapotolewa katika miktadha mbalimbali,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi ya hatua mbili yanayotumiwa katika miktadha mbalimbali,<br>c) kuchangamkia maagizo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maagizo ya hatua mbili,<br>● kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo mepesi ya hatua mbili kwa kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa,<br>● kushiriki katika kutoa na kufuata maagizo mepesi ya hatua mbili,<br>● kufafanua umuhimu wa maagizo,<br>● kuimba nyimbo na kukariri mashairi yanayohusu maagizo kuhusu suala lengwa. | Kufuata maagizo kuna umuhimu gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mjadala na wenzake wakati wa ujifunzaji katika kikundi.<br>• Uwazaji kwa kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa na kufuata maagizo kulingana na yanavyotolewa.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki kuimba nyimbo na pia kukariri mashairi kuhusu maagizo. |
| **Maadili:**<br>• Amani: mwanafunzi anapofanya maigizo katika kikundi na wenzake kwa utulivu.<br>• Haki za kijamii: mwanafunzi anapomtolea mwenzake maagizo yafaayo.<br>• Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake katika kikundi kwa upole na kuelewana. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo ya hatua mbili kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa.<br>● Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaposikiliza vifungu kuhusu sebuleni na vifaa vya sebuleni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kufuata maagizo anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1 Kusoma Kwa Ufahamu:** *Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 43-46 na kutambua msamiati wa suala lengwa ( *runinga, kochi, meza,radio* ) akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma.<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano. | Je, tunawezaje kupata ujumbe katika ufahamu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi vitu vinavyopatikana sebuleni mwao kwa kutumia msamiati aliojifunza. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanapotangamana katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa upendo katika shughuli mbalimbali za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoeleza wenzake kuhusu vitu vya sebuleni. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi na kutambua msamiati wa wa swala lengwa kama zulia, kochi, viti na jinsi ya kuviweka safi ili kuweza kujikinga na maradhi.<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma ufahamu kuhusu sebuleni na vifaa vya sebuleni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Uhariri:**<br><br>*Vipengele katika Uhariri*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuhariri katika maandishi,<br>b) kuhariri maandishi yake baada ya kuyaandika,<br>c) kufurahia kuhariri maandishi baada ya kuyaandika ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuhariri katika maandishi kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kujadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia katika uhariri,<br>● kuipitia kazi yake baada ya kuiandika ili kuhariri tahajia, nafasi baina ya sauti na maneno pamoja na viakifishi kuhusu suala lengwa,<br>● kushirikiana na wenzake kuhariri kazi aliyoandika,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichohariri ili ampe maoni yake. | Je, kwa nini ni vizuri kusoma kazi uliyoandika na kuirekebisha? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapofaulu kuwaonyesha wenzake nafasi baina ya maneno katika kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi akitumia kifaa cha kidijitali.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofaulu kuhariri kifungu cha maneno mawili au sentensi fupi akizingatia nafasi ipasavyo. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli ya kuhariri kifungu cha maneno mawili na sentensi fupi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoandika kifungu kifupi kuhusu shughuli zinazofanywa na familia yao wanapojumuika sebuleni.<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu sebuleni na vifaa vya sebuleni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuhariri anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1**<br>*Ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi katika sentensi,<br>b) kutumia ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi, katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ukanusho wa nafsi ya pili, umoja na wingi, katika kadi maneno, mti maneno kuhusu suala lengwa,<br>• kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi kwenye kifaa cha kidijitali,<br>• kushirikiana na wenzake katika kikundi kukanusha sentensi katika nafsi ya pili, umoja na wingi kuhusu suala lengwa, kwa mfano: *wewe - ulisoma – wewe hukusoma,*<br>• kutunga sentensi zinazoashiria ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi kuhusu suala lengwa kwa kusaidiwa na mwalimu,<br>• kufanya zoezi la kujaza nafasi kwa kutumia nafsi ya pili, umoja na wingi, kwenye kifaa cha kidijitali, | Ukanushaji wa sentensi katika umoja na wingi unahusu nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizokanusha katika nafsi ya pili, umoja na wingi ili ampe maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kumtungia mwenzake sentensi katika kikundi kwa kutumia nafsi ya pili umoja na wingi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza vitendo vinavyoashiria nafsi ya pili umoja na wingi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposikiliza kifungu au wimbo kuhusu ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi kwenye kifaa cha kidijitali.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi zinazoashiria ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake wanapotungiana sentensi kwenye kikundi kwa kutumia ukanusho wa nafsi ya pili umoja na wingi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kukanusha sentensi zilizo katika nafsi ya pili umoja na wingi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala mtambuko:**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapofanya shughuli ya ukanusho wa nafsi ya pili katika umoja na wingi kuhusu suala lengwa akizingatia hatua za kiusalama katika mtandao.
- Utunzi na usalama watoto: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nafsi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

## 8.0 USALAMA WANGU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwaa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Sauti: /sh/, /th/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno na sentensi zenye sauti lengwa,<br>b) kutamka maneno na sentensi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa katika matini mbalimbali kama vile kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza pamoja na mwalimu na mwishowe kutamka akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye sauti lengwa na zinazolenga suala lengwa zikitamkwa | Unajua kutamka maneno gani yenye sauti /*sh*/ na /*th/*? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kuzitambua,<br>● kusikiliza na kusimulia kifungu cha hadithi kuhusu suala lengwa (*k.v usalama wangu na jinsi ya kudumisha usalama barabaran),*<br>● kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno na sentensi zenye sauti lengwa na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi bora. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisimulia kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka sauti lengwa ipasavyo.

**Maadili:**

- Umoja: wanafunzi wanaposhirikiana katika vikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za vikundi.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko:**<br>● Utunzi wa usalama wa watoto: mwanafunzi anaposikilia kifungu cha hadithi kinacholenga mada lengwa na kutambua maneno yenye sauti /*sh*/na /*th/*.<br>● Magonjwa yanayosababishwa na mitindo ya maisha: mwanafunzi anaposikiliza kifungu kinacholenga suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa ufasaha**<br><br>***Sauti:*** ***/sh/ na /th/***<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akishirikiana na wenzake kuhusu suala lengwa,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo *(maneno 42 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi)* akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kifungu cha hadithi kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijtali, akishirikiana na wenzake kuhusu usalama wangu na jinsi ya | Je, unajua kusoma maneno gani yenye sauti<br>*/sh/* na */th/*? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kudumisha usalama barabarani, akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoendelea kusoma sentensi na vifungu mbalimbali vyenye sauti lengwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake kwenye kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia.

**Masuala mtambuko:**

- Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaposoma kifungu kinachohusu suala lengwa, anakuza ujuzi wake kuhusu masuala ya usalama.
- Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma vifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma vifungu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Tahajia**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi za maneno katika sentensi,<br>b) kuandika sentensi akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>c) kufurahia kutumia tahajia sahihi katika maandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua tahajia sahihi za maneno katika sentensi kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili kuhusu tahajia sahihi ya maneno kwenye kifungu kitabuni au kifaa cha kidijitali,<br>• kuandika sentensi kuhusu suala lengwa akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>• kurekebisha sentensi akizingatia tahajia sahihi,<br>• kujaza nafasi kwenye kifungu akizingatia tahajia sahihi kuhusu suala lengwa,<br>• kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizotunga akizingatia tahajia sahihi ili ampe maoni. | Je, kwa nini ni vizuri kuandika maneno kwa kuzingatia tahajia ifaayo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuchangia kikamilifu katika kutambua na kuandika akizingatia tahajia sahihi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika sentensi zinazozingatia tahajia akitumia kifaa cha kidijitali.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofaulu kutumia tahajia sahihi katika sentensi. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Usalama wa watoto barabarani: mwanafunzi anapotambua tahajia sahihi za maneno katika sentensi kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali akizingatia mada lengwa.<br>• Haki za watoto: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya tahajia anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Matumizi ya huu na hii**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua **huu** na **hii** katika vifungu,<br>a) kutumia **huu** na **hii** kutajia vitu katika mazingira yake,<br>b) kuchangamkia matumizi ya **huu** na **hii** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno **huu** na **hii** kwa kutumia nyenzo kama vile kadi maneno, mti maneno, chati au kifaa cha kidijitali,<br>● kusoma vifungu vinavyojumuisha **huu** na **hii,**<br>● kuonyesha vitu mbalimbali kuhusu suala lengwa kama vile miti na kuvitungia sentensi katika kikundi (k.m *Mti huu – miti hii,)*<br>● kukamilisha vifungu vyenye nafasi kwa kutumia **huu** na **hii** akishirikiana na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia **huu** na **hii** na zinazolenga suala lengwa**,**<br>kuandika vifungu akitumia **huu** na **hii** kutokana na picha. | Ni vitu gani unavyoweza kurejelea kwa kutumia maneno **huu** na **hii**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua maneno **huu** na **hii** na kutunga sentensi akiyatumia.<br>● Hamu ya ujifunzaji: anapomshirikisha mzazi au mlezi wake kurejelea vitu vinavyopatikana nyumbani kwa kutumia maneno **huu** na **hii** ipasavyo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kiteknolojia kujifunzia. |
| **Maadili:**<br>Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Magonjwa ya kuambukizwa na yasiyoambukizwa: mwanafunzi anapoandika kifungu chepesi kuhusu usalama wangu akitumia **huu** na **hii** kutokana na picha ipasavyo.<br>• Haki za watoto: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya sarufi kuhusu vionyeshi anavyojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* *na Indigenous Language Activities*. |

## 9.0 HOSPITALINI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo ya papo kwa hapo.**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuonyesha ufahamu wa suala linalozungumziwa,<br>b) kuzingatia matamshi bora anapozungumza,<br>c) kujieleza kwa ufasaha wakati wa kuzungumza, kutumia viziada lugha ipasavyo wakati wa kuzungumza,<br>d) kufurahia kutoa mazungumzo ya papo kwa hapo ili kujenga ufasaha wa kuzungumza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kuonyesha ufahamu wa suala lengwa kwa kulieleza ipasavyo,<br>● kusikiliza mgeni mwalikwa au mwalimu, wakizungumza,<br>● kushirikiana na wenzake kusikiliza mazungumzo kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa,<br>● kuzungumza kwa kutamka ipasavyo sauti na maneno,<br>● kujieleza kwa ufasaha anapozungumza kwa kutumia lugha inayoeleweka kuhusu suala lengwa, kutumia sauti ipasavyo kwa kuzingatia sauti inayosikika, kasi ya kuzungumza, toni pamoja na udhibiti wa upumuaji na viungo vya kutamka,<br>● kuzungumza akitumia ipasavyo viziada lugha kama vile muktadha wa mazungumzo, | Tunazingatia mambo gani tunapozungumza papo kwa hapo? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>ishara za uso, mikono mtuo, mkao wa mwili, utazamaji hadhira kuhusu suala lengwa,<br>● kushirikiana na wenzake kuwasilisha mazungumzo ya papo kwa hapo wakiwa na wenzake, au wakati wa mazungumzo ya hadhara katika tamasha za muziki.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuwasilisha hoja zake.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofanikiwa kuwasilisha mazungumzo yake ifaavyo mbele ya wenzake.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kijiditali kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa,<br>• Uraia: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapatia wenzake nafasi kushiriki katika majadiliano.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali na kukitunza ipasavyo.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>● Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusikiliza mazungumzo yanayohusu afya na jinsi ya kuepuka maradhi mbalimbali.<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya mazungumzo ya papo kwaa hapo anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji<br>wa stadi hiyo katika somo la English Language Activities  na Indigenous Language Activities.</td></tr>
</table>

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br><br>*Kusoma kifungu*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kutabiri yatakayotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>c) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 47 - 50 na kutambua msamiati wa suala lengwa (*dawa, sindano, kitanda*) akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu akiwa peke yake, au na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma, | Je, ukitaka kupata ujumbe kwenye kifungu unazingatia nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe na mafunzo katika kifungu cha ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomhadithia mzazi au mlezi kifungu alichokisoma shuleni kuhusu suala lengwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanaposhiriki katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowajali wenzake katika kikundi na kuwapa nafasi ya kushiriki.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi cha ufahamu kuhusu suala lengwa.
- Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

<table>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo maalum Yanayotarajiwa</th><th>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</th><th>Swali Dadisi Lililopendekezwa</th></tr>
<tr><td>9.3 Kuandika</td><td>9.3.1 Kuandika Kifungu<br><br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala la kuandikia kifungu,<br>b) kuandika kifungu kifupi kutokana na mazingira yake,<br>c) kufurahia kuandika kifungu ili kujieleza.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua suala la kuandikia kwa kulijadiliana na wenzake darasani,<br>• kutazama picha kuhusu suala lengwa ili kupata habari za kuandikia,<br>• kuwaelekeza wenzake kuhusu atakachoandikia akiwa na wenzake,<br>• kusikiliza wenzake wakieleza kuhusu jambo au suala watakaloandikia kuhusu suala lengwa,<br>• kuandika kifungu kifupi cha sentensi moja au zaidi chenye maelezo yanayoeleweka kuhusu suala lengwa,<br>• kuwawasilishia wenzake kifungu alichoandika ili wakitolee maoni,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokiandika na kumweleza suala aliloandikia ili ampe maoni.</td><td>Je, unaongozwa na mambo gani unapotaka kuandika kifungu?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu suala la kuandikia.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kutumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi na kujadili suala analoliandikia.</td></tr>
</table>

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika kifungu kifupi kutokana na mazingira yanayohusu suala lengwa.<br>● Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapoandika kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika kifungu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* *na Indigenous Language Activities.* |

## 9.0 HOSPITALINI

<table>
<tr><th>Mada</th><th>Mada Ndogo</th><th>Matokeo maalum Yanayotarajiwa</th><th>Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa</th><th>Swali Dadisi Lililopendekezwa</th></tr>
<tr><td>9.4 Sarufi</td><td>9.4.1 Matumizi ya Vizuri na Vibaya, Polepole na Haraka.<br><br>(Vipindi 3)</td><td>Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi yafaayo ya vizuri na vibaya, polepole na haraka katika kifungu,<br>b) kutumia vizuri na vibaya, polepole na haraka katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya vizuri na vibaya katika kuimarisha mawasiliano.</td><td>Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua matumizi ya vizuri na vibaya, polepole na haraka katika nyenzo kama vile kadi za majina, kapu maneno, mti maneno au chati au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>• kuigiza vitendo mbalimbali kwa kutumia vizuri na vibaya, polepole na haraka,<br>• kuandika sentensi zinazojumuisha vizuri na vibaya, polepole na haraka,<br>• kujaza nafasi kwa kutumia vizuri na vibaya, polepole na haraka akizingatia suala lengwa kwa kusaidiwa na mwalimu.</td><td>Unatumia maneno yapi kuelezea jinsi watu wanavyofanya vitendo?</td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia vizuri na vibaya, polepole na haraka.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya vizuri na vibaya, polepole na haraka akishirikiana na wenzake katika kikundi.</td></tr>
</table>

- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka**.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasiliana na mzazi au mlezi kwa kutumia vielezi **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** kurejelea vitendo anavyofanya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **vizuri** na **vibaya**, **polepol**e na **haraka**.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuwasiliana na mzazi au mlezi kwa kutumia vielezi **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** kurejelea vitendo anavyofanya nyumbani.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapotumia **vizuri** na **vibaya**, **polepole** na **haraka** kutunga sentensi akizingatia suala lengwa.
- Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapotunga sentensi kwa kuzingatia suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kutumia maneno ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.*

## 10.0 HALI YA ANGA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Alfabeti ya Kiswahili.*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti mbalimbali za Kiswahili kwa ufasaha,<br>c) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti za alfabeti ya Kiswahili katika matini mbalimbali au kifaa cha kidijitali,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti mbalimbali za Kiswahili yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali yanayolenga suala lengwa,<br>● kutamka pamoja na mwalimu maneno aliyosikiliza, kisha ayaseme akishirikiana na wenzake akilenga suala lengwa,<br>● kuunganisha silabi ili kusoma maneno yanayotokana na sauti mbalimbali,<br>● kujirekodi akisoma maneno yenye sauti mbalimbali za Kiswahili na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi bora. | Unazingatia nini kutamka sauti za Kiswahili kikamilifu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti mbalimbali.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti mbalimbali.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotambua sauti za alfabeti ya Kiswahili katika matini mbalimbali kuhusu suala lengwa.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapotumia maneno yanayolenga suala mtambuko. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa ufasaha**<br><br>*Kusoma kifungu.*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti mbalimbali za alfabeti ya Kiswahili katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti mbalimbali za Kiswahili katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kwenye kifaa cha kidijitali kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa sauti inayosikika akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 45 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*) akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake, | Kusoma kifungu kwa ufasaha unazingatia mambo gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | • kuwawasilishia hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k akishirikiana na wenzake akizingatia sauti inayosikika, matamshi bora, kasi na ishara zifaazo,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi alichosoma shuleni kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuwasilisha kifungu cha hadithi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi walichosoma shuleni kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi na ishara zifaazo.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutekeleza shughuli mbalimbali za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposoma vifungu vinavyolenga suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Maneno Na Sentensi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye matini mbalimbali,<br>b) kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu yanayohusu suala lengwa,<br>c) kuandika sentensi fupi zinazohusu suala lengwa,<br>d) kufurahia kuandika ipasavyo maneno na sentensi kutokana na imla. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno mepesi ya silabi tatu kwenye matini mbalimbali,<br>● kuandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu kitabuni au katika kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika maneno mepesi ya silabi tatu,<br>● kushiriki mchezo wa kuandika maneno na sentensi za imla zinayolenga suala lengwa akiwa na wenzake<br>● kuwawasilishia wenzake maneno ya imla ili kuyaandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika maneno atakayosomewa na wenzake daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika daftarini sentensi sahili walizotunga zinazolenga suala lengwa. | Sentensi sahili ni sentensi za aina gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia kikamilifu kutambua maneno ya silabi tatu katika sentensi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika maneno atakayosomewa na wenzake<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoandika sentensi za imla akishirikiana na mzazi au mlezi kwenye kifaa cha kidijitali na kuwatumia wenzake mtandaoni.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuunda sentensi nyepesi. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika maneno mepesi ya imla ya silabi tatu yanayohusu suala lengwa.<br>• Magonjwa ya kuambukizwa na yasiyoyakuambukizwa: mwanafunzi anapoandika sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi kuandika maneno na sentensi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities  na Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vitendo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo katika sentensi mbalimbali,<br>b) kutumia majina ya vinyume vya vitendo katika sentensi,<br>c) kuchangamkia kutumia majina ya vinyume vya vitendo katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vinyume vya vitendo katika sentensi katika kadi maneno, kapu maneno, kifungu, chati, kitabu au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake akizingatia suala lengwa,<br>● kusikiliza sentensi zenye vinyume vya vitendo zikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma vinyume vya vitendo katika sentensi vinavyohusu suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa katika sentensi akiwa na wenzake,<br>● kukamilisha sentensi akitumia vinyume vya vitendo akishirikiana na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni, | Je, vinyume vya vitendo huwa vinahusu nini? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizotunga kwa kutumia vinyume vya vitendo ili ampe maoni.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuandika vinyume vya vitendo katika sentensi.</li><li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya teknolojia kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo.</li><li>Ubunifu: anapoigiza matumizi ya vinyume vya vitendo mbalimbali.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<ul><li>Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.</li><li>Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kikundi.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<ul><li>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumika katika sentensi</li><li>Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo vinavyohusiana na hali ya anga.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language Activities.</td></tr>
</table>

**MWONGOZO ULIOPENDEKEZWA WA VIWANGO NA VIGEZO VYA KUTATHMINIA**

**MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| **Viwango Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutumia ishara za mwili ipasavyo katika mawasiliano.** *(kuketi, kusimama na ishara za uso)* | Anatumia ishara za mwili ipasavyo katika mawasiliano kila wakati. | Anatumia ishara za mwili ipasavyo. | Anatumia baadhi ya ishara za mwili ipasavyo. | Anatumia baadhi ya ishara za mwili kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora** (*matamshi ya sauti zinazokaribiana:* **Sauti /p/, /f/, /v, /ch/, /*ny*/, /*ng*/, /sh/, /th/** na alfabeti ya Kiswahili. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa kila wakati. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** *Matamshi, kiimbo na kusikika)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia matamshi bora, kiimbo na sauti inayosikika katika miktadha mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia matamshi bora, kiimbo na sauti inayosikika. | Anazungumza na kujieleza bila ufasaha na kuzingatia baadhi ya matamshi bora, kiimbo na sauti. | Anazungumza na kujieleza bila ufasaha na kuzingatia baadhi ya matamshi bora, kiimbo na sauti kwa kusaidiwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo (***msamiati wa heshima, adabu, maamkuzi, maagano.)* | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano, kutumia msamiati wa heshima na adabu kwa wepesi. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi na maagano, kutumia msamiati wa heshima na adabu. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano, kutumia baadhi ya msamiati wa heshima na adabu. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi na maagano, kutumia baadhi ya msamiati wa heshima na adabu kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutoa ujumbe katika hadithi.** *(msamiati, ujumbe katika hadithi)* | Anatoa ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu kwa utendeti. | Anatoa ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu. | Anatoa baadhi ya ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu.. | Anatoa baadhi ya ujumbe kwenye hadithi aliyosikiliza kikamilifu kwa kusaidiwa. |

**MADA: KUSOMA**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kusoma**. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kusoma kwa uketo. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kusoma. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kusoma. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kusoma kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu - Vifungu.** *( ujumbe, msamiati)* | Anasoma vifungu, kutambua ujumbe na matumizi mwafaka ya msamiati kila wakati. | Anasoma vifungu, kutambua ujumbe na matumizi mwafaka ya msamiati. | Anasoma vifungu, kutambua baadhi ya ujumbe na baadhi ya matumizi mwafaka ya msamiati. | Anasoma vifungu, kutambua baadhi ya ujumbe na baadhi ya matumizi mwafaka ya msamiati kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*matamshi bora*, *kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo akizingatia sauti lengwa.*) *(/p/, /f/, /v/),/ch/,(/ny/ /ng/), (/sh/, /th/)* | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa kuelekezwa. |

**MADA: KUANDIKA**

| Viwango Vigezo | Kuzidi matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuzingatia jinsi ya kuketi na mbinu zifaazo wakati wa kuandika**. *(kuketi wima, kushika kalamu, ipasavyo, kuandika kutoka kushoto hadi kulia n.k)* | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kuandika kila wakati. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia mbinu zifaazo wakati wa kuandika. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kuandika. | Anaketi jinsi ipasavyo na kutumia baadhi ya mbinu zifaazo wakati wa kuandika kwa kusaidiwa. |
| **kuweza kuandika kwa hati nzuri sentensi na kifungu kifupi kwa kuzingatia tahajia na hati nadhifu.** *(herufii ndogo, herufi kubwa)* | Anaan Anaandika kwa hati nadhifu kwa kuzingatia tahajia kila wakati. | Anaandika kwa hati nadhifu kwa kuzingatia tahajia. | Anaandika kwa hati isiyo nadhifu kwa kutozingatia baadhi ya tahajia. | Anaandika kwa hati isiyo nadhifu kwa kutozingatia baadhi ya tahajia kwa kusaidiwa. |
| **kuweza kuzingatia muundo na mtindo wa kuandika na kuhariri sentensi au matini** (uakifishaji ufaao *)* | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu kila wakati. | Anazingatia muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu. | Anazingatia baadhi ya vipengele vya muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu. | Anazingatia baadhi ya vipengele vya muundo na mtindo unaofaa kuandika sentensi au kifungu kwa kusaidiwa. |

**MADA: SARUFI**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia maneno mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.** **(***wewe na nyinyi , huyo na hao, huyu na hawa, ako na enu, refu na kubwa, tamu, vizuri na vibaya, polepole na haraka )* | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya maneno katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya maneno katika matini kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno.** *(Vinyume vya vitenzi)* | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno kwa utendeti. | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia umoja na wingi wa maneno na vifungu vya maneno.vya maneno.** (*umoja, wingi )* | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa maneno kwa utendeti. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa maneno. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa baadhi ya maneno maneno. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa baadhi ya maneno maneno kwa kuelekezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua ukanusho wa nafsi ya pili, uakifishaji unaofaa na vinyume vya vitenzi.** *( ukanushaji wa nafsi ya pili, vinyume vya vitenzi)* | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya pili, na vinyume vya vitenzi kwa wepesi. | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya pili na vinyume vya vitenzi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya pili na vinyume vya vitenzi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya pili na vinyume vya vitenzi kwa kusaidiwa |

# KISWAHILI MAZOEZI YA LUGHA
# GREDI YA 3

## 1.0 UZALENDO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Maamkuzi na Maagano**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>b) kutumia ipasavyo maamkuzi na maagano mbalimbali yatumiwayo katika jamii,<br>c) kuthamini matumizi ya maamkuzi na maagano katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotumiwa katika maamkuzi na maagano *(k.v. Umeamkaje? Umeshindaje? Safiri salama, mchana mwema, usiku mwema)* kutoka kwenye chati, vitabu, kadi maneno, mti maneno, michoro, picha au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kujadili na wenzake picha, michoro, video n.k. zinazoonyesha vitendo vya maamkuzi na maagano,<br>● kuigiza maamkuzi na maagano akiwa na wenzake ili kujenga umilisi wa kutumia maneno haya,<br>● kujadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii yake. | Je, unajua maamkuzi na maagano yapi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuwasiliana na wenzake katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji.<br>● Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli mbalimbali za kikundi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposikiliza kwa makini maamkuzi na maagano mbalimbali kutoka kwenye vifaa vya kidijitali. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika mijadala ya maamkuzi na maagano darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>● Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya heshima na adabu katika maamkuzi na maagano. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapojadiliana na mzazi au mlezi wake maamkuzi na maagano kutoka kwa jamii yake. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maamukuzi na maagano anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno 51- 54 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v. uzalendo, umoja, undugu, ushirikiano, upendo)* akiwa na wenzake,<br>• kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>• kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>• kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>• kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>• kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa ili amtolee maoni. | 1. Je, unapenda kusoma hadithi za aina gani?<br>2. Je, ni mambo gani unayoweza kujifunza kutokana na hadithi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi kutambua msamiati kuhusu suala lengwa.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili picha, kutabiri na kudhibitisha utabiri kuhusu hadithi. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotoa muhtasari wa hadithi aliyoisoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.<br>● Usalama wa mtandaoni: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma ufahamu kuhusu suala lengwa na kuzingatia usalama mtandaoni. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Hati Nadhifu:** *Kifungu*<br><br>**(Vipindi 3**) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu,<br>b) kuandika kifungu cha maneno kati ya 25-30 kwa hati nadhifu,<br>c) kufurahia kuandika kwa hati nadhifu ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mambo mbalimbali yanayozingatiwa kufanikisha hati nadhifu *(k.v. muundo wa herufi, nafasi ifaayo kati ya maneno, nafasi zifaazo pambizoni, kutenganisha sentensi ifaavyo, usafi wa nakala)* kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu cha maneno yasiyozidi 30 kwa hati nadhifu kutoka kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 30 akizingatia hatua za uandishi *(k.v.* | Unazingatia mambo gani unapoandika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake. | |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili mambo ya kuzingatiwa ili kufanikisha hati nadhifu.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli mbalimbali za kuandika.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anaponakili kifungu cha maneno kwa hati nadhifu. | | | | |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali. | | | | |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa. | | | | |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya maandishi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* | | | | |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Matumizi ya Yeye na Wao**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua neno **yeye** na **wao** katika sentensi,<br>b) kutumia neno **yeye** na **wao** ipasavyo katika sentensi,<br>c) kufurahia kutumia neno **yeye** na **wao** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaohusu **yeye** na **wao** kutoka kwa mwalimu au kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua neno **yeye** na **wao** kutoka kifungu alichokisikiliza,<br>● kusoma vifungu na kutambua neno **yeye** na **wao** akiwa na wenzake au katika kikundi,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia **yeye** na **wao,**<br>● kutumia **yeye** na **wao** katika kuigiza mazungumzo na wenzake katika kikundi (k.v.*Yeye anasoma - wao wanasoma).* | Ni maneno gani unayoyatumia kuwataja wenzako bila kutumia majina yao halisi? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutoa mifano kwa kutumia **yeye** na **wao**.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya **yeye** na **wao**.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya **yeye** na **wao**.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoweza kutumia **yeye** na **wao** ifaavyo. | | | | |

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi huku akisikiliza michango yao na kutoa maoni. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maneno lengwa.<br>● Uraia: mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nafsi ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities* |

## 2.0 SHAMBANI

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Matamshi Bora:** *Vokali na Konsonanti za Kiswahili*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vokali za Kiswahili katika matini,<br>b) kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili katika matini,<br>c) kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>d) kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili katika matini,<br>**e)** kuchangamkia kutamka sauti | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vokali za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa,<br>● kutamka ipasavyo vokali za Kiswahili,<br>● kutambua konsonanti za Kiswahili katika matini ya kutamkwa au kuandikwa,<br>● kutamka ipasavyo konsonanti za Kiswahili,<br>● kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili (a, b, ch, d, dh, e, f, g, gh, h, i, j, k, l, m, n, ng, ng’, ny, o, p, r, s, sh, t, th, u, v, w, y, z) zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kutambua vokali na konsonanti,<br>● kutambua vokali na konsonanti za Kiswahili katika kifungu kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutamka maneno, sentensi au kifungu chenye sauti za Kiswahili akiwa na wenzake, | Je, kwa nini ni muhimu kutambua sauti za lugha fulani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | za Kiswahili ili kuboresha matamshi. | ● kujirekodi akitamka sauti za Kiswahili akitumia vifaa vya kidijitali na kujitathmini pamoja au kutathminiwa na wenzake,<br>● kutamka sauti za kiswahili ipasavyo naye mzazi au mlezi ampe maoni yake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuzisikiliza, kuzitambua na kuzitamka vokali na konsonanti za Kiswahili.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza vokali na konsonanti za Kiswahili na kujirekodi akizitamka.
- Kujiamini: mwanafunzi anapozitamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwa mzazi au mlezi wake ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapokuwa makini kusikiliza vokali na konsonanti zikitamkwa na  mwalimu.

**Maadili:**

- Umoja:  mwanafunzi anaposhirikiana na wanzake katika shughuli za kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kwenye kikundi kwa utulivu.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakiwemo walio na changamoto za kimaumbile.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali alivyotumia katika kujirekodi.

**Masuala Mtambuko:**

Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka vokali na konsonanti za Kiswahili kuhusu suala lengwa.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /bw/, /fy/ na /kw/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa *(/bw/, /fy/, /kw/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 47 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*) akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>• kusoma hadithi kutoka kwenye kitabu, kifaa cha kidijtali, n.k. akiwa na wenzake akizingatia | Je, utafanya mambo gani unaposoma ili uweze kusikika vizuri? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>sauti inayosikika, matamshi bora, kasi ifaayo na ishara zifaazo,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusoma kwa ufasaha akiwa na wenzake.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa huku akizingatia matamshi bora, sauti inayosika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua sauti lengwa kwa ufasaha na kutumia vifaa vya kidijitali.<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza kifaa cha kidijitali anachotumia kujifunzia.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>• Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma hadithi yenye sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama.<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu na wenzake kuhusu suala lengwa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language Activities.</td></tr>
</table>

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi kubwa katika matini,<br>b) kuandika kifungu cha hadithi akitumia herufi kubwa ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi kubwa katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua herufi kubwa katika kifungu kilicho kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa,<br>● kuandika kifungu chenye maneno **25-30** akizingatia maumbo ya herufi kubwa ifaavyo akizingatia hatua za uandishi (*maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi)* na kuwasomea wenzake,<br>● kumwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia mpangilio ufaao wa herufi kubwa ili akitolee maoni. | Kwa nini tunatumia hati nadhifu katika uandishi? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kuandika kifungu kwa kutumia herufi kubwa. | | | | |

| |
|---|
| • Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia maumbo ya herufi kubwa kwenye kifaa cha kidijitali.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi wake kifungu alichokiandika akitumia maumbo ya herufi kubwa.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika maumbo ya herufi kubwa ipasavyo. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika kifungu.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana kwa utulivu na wenzake kutathmini herufi kubwa alizoziandika. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Masuala ya kijamii na kiuchumi: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia herufi kubwa ipasavyo. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika herufi kubwa anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kutunga sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>• kusoma sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>• kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>• kuambatanishe umoja na wingi wa sentensi alizopewa kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali, n.k akiwa na wenzake,<br>• kuigiza michezo inayohusisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na wenzake,<br>• kutunga sentensi katika umoja na wingi wa sentensi akiwa na wenzake,<br>• kuwasiliana na mzazi au mlezi akitumia sentensi katika hali ya umoja na wingi ipasavyo. | Je, kwa nini unahitaji kutaja vitu katika hali ya umoja na wingi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika kuandika sentensi katika umoja na wingi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoeleza kuhusu vitu katika mazingira yake katika umoja na wingi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi katika umoja na wingi. |
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma sentensi katika hali ya umoja na wingi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza nyenzo zinazotumiwa katika ujifunzaji wa sentensi za umoja na wingi.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi akizingatia suala lengwa.<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine wanapotambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye matini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nomino katika sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

## 3.0 MIEZI YA MWAKA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Maneno ya Heshima na Adabu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno ya heshima na adabu katika matini,<br>b) kutumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano,<br>c) kuthamini matumizi ya maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama michoro, picha au video inayowasilisha vitendo vya heshima na adabu akiwa na wenzake,<br>● kutambua maneno ya adabu na heshima kutoka kwa michoro, picha au video aliyotazama (tasfida) (*k.v. kwenda msalani*, *haja kubwa*, *haja ndogo*, *kuendesha),*<br>● kuigiza mazungumzo yanayoonyesha matumizi ya maneno ya heshima na adabu akishirikiana na wenzake,<br>● kujadiliana na mzazi au mlezi maneno ya heshima na adabu katika jamii yake. | Je, ni kwa nini tunatumia maneno ya heshima na adabu katika mawasiliano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika majadiliano kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama picha, michoro na video kuhusu maneno heshima na adabu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza kuhusu matumizi ya maneno ya heshima na adabu.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua baadhi ya maneno ya adabu na heshima na matumizi yake. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapotumia maneno ya adabu na heshima ipasavyo.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali ipasavyo.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika maigizo ya mazungumzo ya maneno ya adabu na heshima. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuigiza maneno ya heshima na adabu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya heshima na adabu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na miezi ya mwaka inayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 55 - 60 na kutambua msamiati wa suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kufafanua mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>● kumsomea mzazi au mlezi majina ya miezi ya mwaka aliyojifunza ili amtolee maoni. | Je, ni mambo yapi unaweza kujifunza kutokana na unachokisoma? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu katika kutabiri kitakachotokea katika hadithi.<br>• Uraia: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi kueleza ujumbe wa kifungu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma na kutoa utabiri katika kifungu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe katika kifungu.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anachotumia kujifunzia. Pia anapotekeleza majukumu aliyopewa anapofanya maigizo kuhusu miezi ya mwaka.<br>• Haki za kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuimba nyimbo kuhusu suala lengwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijami: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya maigizo kuhusu majina ya miezi ya mwaka ukakamavu wake unajengeka. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na miezi ya mwaka inayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Hati Nadhifu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ipasavyo katika kifungu,<br>b) kuandika kifungu akitumia herufi ndogo ifaavyo,<br>c) kufurahia kuandika kwa kuzingatia herufi ndogo ifaavyo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutazama mfano wa uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kutambua herufi ndogo zilizoandikwa ifaavyo katika kifungu kilicho kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kunakili kifungu akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>● kuandika kifungu chenye maneno 55-60 akizingatia maumbo ya herufi ndogo ifaavyo akizingatia hatua za uandishi *(maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji,*<br>*nakala safi)* na kuwasomea wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>● kuwaonyesha wenzake kifungu alichoandika akizingatia maumbo ya herufi ndogo ili waitolee maoni. | Je, unazingatia mambo gani unapoandika herufi ndogo ifaavyo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili na wenzake kuhusu jinsi ya kuendeleza herufi ndogo.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kutumia kifaa cha kidijitali kutazama kielelezo cha uendelezaji ufaao wa maumbo ya herufi ndogo.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi akizingatia mwendelezo ufaao wa herufi ndogo,<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowaonyesha wenzake kazi aliyoandika ili waitolee maoni. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu mada lengwa kwa kutumia herufi ndogo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za kikundi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na miezi ya mwaka inayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Matumizi ya Maneno Yule na Wale**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **yule** na **wale** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya neno **yule** na **wale** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya neno **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vyombo vya kidijitali nk. akiwa na wenzake,<br>● kusilikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya neno **yule** na **wale** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kujadili matumizi yake akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zilizotumia neno **yule** na **wale** kutoka kwenye chati, kitabu, vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kuigiza vitendo vya kuwaashiria watu mbalimbali kwa kutumia neno **yule** na **wale** akiwa na wenzake,<br>● kuandika sentensi akitumia **yule** na **wale (***k.v Mtoto yule anacheza - watoto wale wanacheza)* na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili akamilishe sentensi akitumia **yule** na **wale,**<br>● kumsomea mzazi au mlezi kazi aliyoandika kuhusu matumizi ya **yule** na **wale.** | Unaweza kutunga sentensi zipi ukitumia maneno **yule** na **wale**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kumtungia mwenzake sentensi akitumia maneno **yule** na **wale**.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza matumizi ya neno **yule** na **wale** akishirikiana na wenzake katika kikundi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia neno **yule** na **wale** kwa lugha fasaha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kwa kutumia neno **yule** na **wale**. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu mchango wa wenzake katika kazi ya kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia neno **yeye** na **wao.**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

## 4.0 KAZI MBALIMBALI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Silabi za sauti /py/, /vy/ na /sh/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini,<br>d) kufurahia matamshi bora katika awasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/py/, /vy/, /sh/)* katika matini mbalimbali (*k.v kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali),*<br>● kutumia kifaa cha kidijitali *(k.v. kupitia programu ya papaya)* kusikiliza matamshi bora ya sauti lengwa,<br>● kusikiliza silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwa vifaa vya kidijitali (*k.v. kinasasauti na rununu)* akiwa na wenzake kisha azitamke, | Unazingatia mambo gani unapotamka maneno mbalimbali katika kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusikiliza maneno yenye sauti lengwa yakisomwa na mwalimu kisha atambue sauti lengwa katika maneno hayo,<br>• kutamka maneno yenye sauti ifaavyo akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kutoka kwa kitabu au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anashirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake wa jamii mbalimbali katika kutekeleza shughuli za kikundi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana katika kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu katika kutambua silabi za sauti lengwa.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutoka sehemu mbalimbali kusoma kifungu chenye maneno ya sauti /*py/*, */vy/* na */sh/* kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma na kutunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matamshi bora anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4. 2.1 Kusoma kwa Ufasaha.**<br>*Sauti /py/, /vy/, /sh/)*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti lengwa (*/py/, /vy/, /sh/)* katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 49 kwa dakika na kwa kuizingatia viakifishi*) akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake, | Je, unahakikishaje umesoma kifungu kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | ● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika kutambua sauti lengwa na kusoma kifungu.
- Uraia: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kusoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sauti lengwa katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa.
- Kujithamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akitumia matamshi bora sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu cha maneno yenye sauti lengwa.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la mieza ya mwaka na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Nafasi ya Pambizo katika Uandishi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya,<br>b) kuandika kifungu cha maneno yasiyozidi 60 akizingatia pambizo na aya,<br>c) kufurahia kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua nafasi ya pambizo na nafasi ya kuzingatia anapoandika aya akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu na kutambua pambizo na aya kwenye kitabu, chati, kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kuandika kifungu akizingatia pambizo na aya kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali na kuwasomea wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake,<br>● kuandika na kumuonyesha mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ili ampe maoni yake. | Je, kwa nini tuzingatie nafasi za pambizo tunapoandika? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu akizingatia aya na pambizo.

| |
|---|
| ● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi kifungu alichoandika akizingatia aya na pambizo ipasavyo.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoandika kifungu akizingatia aya na pambizo na kuwasomea wenzake. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.<br>● Uzalendo: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kuandika kifungu kifupi akizingatia aya na pambizo. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia pambizo na aya.<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi na wenzake kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika kwa kuzingatia pambizo anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Umoja na Wingi wa Sentensi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sentensi katika umoja na wingi,<br>b) kuandika sentensi katika umoja na wingi,<br>c) kuchangamkia kutumia umoja na wingi katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma sentensi katika umoja na wingi akishirikiana na wenzake,<br>● kutambua sentensi katika umoja na wingi kutoka kwenye chati au vifaa vya kidijitali,<br>● kujaza nafasi kwa kukamilisha sentensi katika umoja na wingi akiwa na mwenzake,<br>● kushiriki katika mchezo wa kusoma sentensi katika umoja na wingi na mwenzake,<br>● kuandika umoja na wingi wa sentensi akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizoandika katika umoja na wingi ili azitolee maoni. | Je, utajua vipi kama sentensi imeandikwa katika umoja au wingi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika sentensi katika umoja na wingi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapokamilisha sentensi katika umoja na wingi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi sentensi alizoandika katika umoja na wingi.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi katika umoja na wingi.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapoandika umoja na wingi wa sentensi.<br>● Haki za jamii: mwanafunzi aanaposhiriki katika mchezo wa kutunga sentensi kwa umoja na wingi na wenzake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotambua sentensi katika umoja na wingi zinazohusiana na mapato ya watu na kazi mbalimbali. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana y umoja na wingi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

## 5.0 USALAMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Ufahamu wa Kusikiliza**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaowasilishwa katika kifungu,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika kifungu alichosikiliza,<br>c) kutunga sentensi kwa kutumia msamiati uliotumika kwenye kifungu alichosikiliza,<br>d) kusimulia upya kifungu cha hadithi winalichokisikiliza,<br>e) kuchangamkia kusikiliza kifungu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kifungu cha maneno 60-65 kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali ili kutambua ujumbe unaowasilishwa,<br>● kutunga sentensi kwa kutumia msamiati aliousikiliza kwenye kifungu,<br>● kujibu maswali yanayohusiana na kifungu alichosikiliza,<br>● kujadili mambo muhimu katika kifungu alichokisikiliza akiwa na wenzake,<br>● kusimulia wenzake upya kifungu alichokisikiliza. | Je, unazingatia mambo gani ili kuelewa mambo unayoelezewa? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na kuwasiliana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika ujifunzaji.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za huduma kwa jamii kwa kusimulia visa vyepesi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anaposimulia upya kifungu alichokisikiliza. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposimulia wenzake upya kifungu alichokisoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposikiliza na kuzungumzia masuala ya usalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 60 - 65 na kutambua msamiati wa suala lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika hadithi akizingatia picha kwenye kifungu,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu, vifaa vya kidijitali au chati akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi baada ya kuisoma,<br>● kufafanua mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu usalama wake shuleni. | Je, ni mambo gani unapaswa kuzingatia ili kufanikisha usomaji bora? |

- **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika kazi za kikundi wanapojadili ujumbe wa kifungu na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunzia.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma matini mbalimbali ili kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia msamiati wa suala lengwa.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadiliana kuhusu ujumbe katika kifungu.
- Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake wanaposhirikiana kusoma kifungu na kutabiri.
- Uadilifu: mwanafunzi anapowashirikisha wengine kufanya maigizo kuhusu usalama shuleni.

**Masuala mtambuko:**

- Mshikamano wa jamii: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika shughuli za kikundi na kutoa mchango wake, ukakamavu wake unajengeka.
- Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu masuala ya usalama.

**Uhusiano na masomo mengine:**

Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufahamu anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Matumizi ya Kiulizi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua alama ya kiulizi katika maandishi,<br>b) kueleza matumizi ya alama ya kiulizi katika maandishi,<br>c) kuandika kifungu cha maneno kati ya 55-60 akitumia alama ya kiulizi ipasavyo,<br>d) kufurahia kutumia kiulizi katika maandishi ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua alama ya kiulizi kutoka kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kujadili na wenzake matumizi ya alama ya kiulizi ili kukuza uwezo wa kuitumia ipasavyo,<br>● kunakili ipasavyo kifungu kilichotumia alama ya kiulizi akishirikiana na wenzake,<br>● kuandika kifungu cha maneno kati ya 55-60 akizingatia matumizi ya alama ya kiulizi kuhusu suala lengwa, na jinsi ya kuzingatia alama za usalama barabarani kisha kuwasomea wenzake ili waitolee maoni. | Je, alama ya kiulizi inatumika vipi katika uandishi? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea kifungu alichoandika kwa kutumia alama kiulizi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu kwa kutumia alama ya kiulizi ipasavyo. | | | | |

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia alama ya kiulizi katika maandishi na pia anapotumia vifaa vya kidijitali. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoelekezwa kutangamana na mitandao ya kijamii kwa njia salama.<br>● Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika kifungu chepesi kuhusu suala la usalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matumizi ya kiulizi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1. Matumizi ya -ake na ao.**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **-ake** na **-ao** katika mawasiliano,<br>b) kutumia **-ake** na **-ao** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia -**ake** na **-ao** ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya -**ake** na –**ao** kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno au chati akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia –**ake** na –**ao** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa, au vifaa vya kidijitali,<br>● kusoma kifungu kilichotumia **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake,<br>● kuigiza matumizi ya **-ake** na **-ao** akiwa na wenzake katika kikundi kwa kutumia vitu anavyomiliki (*k.v kiti chake – viti vyao),*<br>● kutunga sentensi akitumia -**ak**e na -**ao** na kuzijadili na mwenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **-ake** na**-ao,**<br>● kumtungia mzazi au mlezi sentensi zilizo na **-ake** na **-ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani. | Je, -**ake** na -**ao** hutumiwa vipi katika mawasiliano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi akitumia **-ake** na **-ao**.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutumia **-ake** na **–ao** kwa kurejelea vitu mbalimbali nyumbani.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu matumizi ya**-ake** na **-ao**.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi kwa kutumia **-ake** na **-ao**. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu michango ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Masuala ya usalama: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia **-ake** na **-ao**. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sarufi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.* |

## 6.0 USAFI WA MAZINGIRA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*silabi za sauti /dh/, /th/ na /ch/*<br><br>(**Vipindi 3**) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifungu kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye sauti lengwa katika matini,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (*/dh/*, */th/* na */ch/*) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno, vifaa vya kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>● kuambatanisha silabi na kutamka maneno yanayotokana na sauti lengwa akiwa na wenzake, | 1. Je, matamshi bora hufanikisha vipi mawasiliano?<br>2. Je, ni mambo gani yanayozingatiwa ili kuboresha matamshi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>• kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa,<br>• kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa na kusikiliza na wenzake ili kuitathmini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapoambatanisha silabi na kusoma maneno yanayotokana na sauti lengwa.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Haki za jamii: mwanafunzi aposhirikiana na wenzake katika kutamka maneno ya silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>● Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa utulivu kupotambua silabi za sauti lengwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu kifupi kinachohusu usafi wa mazingira akizingatia silabi za sauti lengwa na matamshi bora.<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /dh/, /th/ na /ch/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (*/dh/, /th/ na /ch/*) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 51 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*),<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa | Je, utafanya nini ili kusikika vizuri unaposoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuzingatia ishara zifaazo akishirikiana na wenzake,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchangia katika kutambua sauti na kusoma kifungu.
- Uraia: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi bila ubaguzi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kifungu cha maneno kuhusu suala lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma hadithi kwa kutumia matamshi bora.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali kusoma hadithi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo *la English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Imla**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yanayotamkwa kwenye imla ili kuyaandika ipasavyo,<br>b) kuandika kifungu cha maneno 55-60 yanayotamkwa kwenye imla akizingatia kanuni za uandishi zifaazo,<br>c) kuchangamkia kuandika kifungu akitumia maneno yanayotamkwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za uandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yanayotamkwa yakizingatia suala na sauti */dh/*, */th/* na */ch/* na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali kutoka kwenye kitabu, chati, kapu la maneno n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini maneno yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali ili kuyaandika ipasavyo,<br>kuandika kifungu cha maneno 55-60 yatakayotamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali n.k. akizingatia kanuni zifaazo za uandishi,<br>● kujadili na wenzake kifungu alichokiandika ili kukitathmini,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokiandika akizingatia kanuni za uandishi zifaazo. | Unaposomewa chochote ili ukiandike, utafanya nini ili uandike ifaavyo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowaeleza wenzake maneno katika kifungu cha imla.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapofaulu kuandika kifungu cha imla akitumia kifaa cha kidijitali.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kuandika maneno na kifungu cha imla.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika imla kwa kutumia maneno yenye sauti lengwa. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno 55-60 yatakayotamkwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabianchi: mwanafunzi anapoandika kifungu cha maneno yatakayotamkwa kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kanuni zifaazo za maandishi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika imla anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo *la English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Matumizi ya -eupe, -eusi na -ekundu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maneno yenye **-eupe, -eusi** na **-ekundu** ili kuyatumia ipasavyo katika mawasiliano,<br>b) kutumia**-eupe, -eusi, -ekundu** katika sentensi ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kufurahia kutumia **-eupe, -eusi, -ekundu** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maneno yenye -**eupe, - eusi, -ekundu** kwa kurejelea vitu halisi katika mazingira yake, kitabu, chati, vifaa vya kidijitali n.k. akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maelezo kuhusu matumizi ya, **-eupe, -eusi, -ekundu** kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zinazotumia maneno yenye **-eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zenye matumizi ya -**eupe, -eusi, -ekundu** akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga. | Je, vitu katika mazingira yako yana rangi gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia **-eupe**, **-eusi**, **-ekundu** akiwa na wenzake kutunga sentensi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza matumizi ya **-eupe**, **-eusi**,<br>• **ekundu**.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga akitumia **-eupe**, **-eusi**, **-ekundu**.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotumia maneno yenye **-eupe**, **-eusi**, **-ekundu** kutunga sentensi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kwa heshima katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotekeleza shughuli za darasani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi na kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa mazingira na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

## 7.0 DUKANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Maagizo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maagizo mepesi yanapotolewa darasani,<br>b) kutoa na kufuata maagizo mepesi yanayotumiwa darasani,<br>c) kufurahia kuzingatia maagizo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua aina mbalimbali za maagizo kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kushirikiana na wenzake katika kutoa na kufuata maagizo mepesi kama vile (*k.v. simama uende uufungue mlango),*<br>● kutazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua aina mbalimbali za maagizo akiwa na wenzake,<br>● kuimba nyimbo na kukariri mashairi mepesi yanayohusu maagizo akiwa na wenzake,<br>● kumwimbia mzazi au mlezi wake wimbo unaoashiria maagizo ili atoe maoni yake. | Je,ni kwa nini mtu hufuata yale anayoambiwa? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika masimulizi na wenzake ya kufuata na kutofuata maagizo.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa maoni katika majadiliano kuhusu jinsi ya kufuata maagizo.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza maagizo mepesi akishirikiana na wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Amani: mwanafunzi anapofanya kazi katika kikundi na wenzake kwa utulivu.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali.<br>• Uadilifu: mwanafunzi anapotazama video ya jinsi ya kutoa na kufuata maagizo kutoka kwenye kifaa cha kidijitali bila usimamizi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu matumizi ya pesa dukani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo *la English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities*. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2. Kusoma** | **7.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya ufahamu ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 65 - 70 na kutambua msamiati wa suala lengwa *(k.v duka, bidhaa, pesa, uza, nunua, chenji, mteja, muuzaji)* akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake,<br>● kutabiri ujumbe wa kifungu kwa kutazama picha kwenye kitabu akiwa na wenzake,<br>● kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi akizingatia picha akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu kifungu baada ya kukisoma,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha ufahamu akiwa na wenzake. | Je, unazingatia mambo gani unaposoma kifungu cha hadithi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi ya kikundi na kushiriki kikamilifu wanapotabiri na kujadili ujumbe katika kifungu.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotoa na kuthibitisha utabiri wake kuhusu kitakachotokea katika hadithi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili picha na kutabiri kitakachotokea katika hadithi.<br>• Haki za kijamii: mwanafunzi anapowapa wenzake fursa ya kujieleza katika shughuli za kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotabiri kilichotokea katika kifungu alichokisoma. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu masuala yanayohusiana na shughuli za dukani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Uandishi wa Insha**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika kisa cha kati ya maneno 85-90 kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kufurahia uandishi wa visa tofauti ili kuimarisha mawasiliano andishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa kisa *(k.v. wahusika, ujumbe, muundo),*<br>● kusikiliza kisa kikitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>● kusoma kielelezo cha insha kwenye kitabu, chati au katika kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutambua kanuni muhimu za uandishi (*k.v. hati nadhifu, maudhui, mtiririko n.k.*),<br>● kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na kujadili na wenzake; kisa hiki kifuate hatua tano za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake,<br>● kumsomea kifungu kisha amwonyeshe mzazi au mlezi. | Je, ni mambo gani tunazingatia katika uandishi wa insha? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kujadili na wenzake kutambua vipengele vya uandishi wa insha.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika insha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kuandika kifungu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa na kujadili na wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuheshimu maoni yao.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mahusiano ya kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake na kushirikiana katika shughuli za uhariri.<br>• Masuala ya kifedha: mwanafunzi anapoandika ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya uandishi wa insha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Ukanushaji wa nafsi ya tatu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi,<br>b) kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi kwa usahihi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwenye kadi maneno, mti maneno, kapu maneno, chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali na kutambua ukanushaji wa nafsi hiyo,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja na wingi katika sentensi,<br>● kutunga sentensi akitumia nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji wake (*kwa mfano: yeye anaandika - yeye haandiki),*<br>● kuigiza matumizi ya nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi sentensi za nafsi ya tatu umoja na wingi zilizokanushwa kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. | Unafikiri mwalimu wako alifanya nini jana? Iwapo hakufanya mambo uliyotaja ungesemaje? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu umoja na wingi na ukanushaji wake.<br>• Ujuzi wa kidijitali: wanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi kutumia ukanushaji wa nafsi ya tatu umoja |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza wimbo au kifungu kuhusu ukanushaji wa nafsi ya tatu.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi kwa kutumia nafsi ya tatu katika shughuli za kikundi.<br>• Haki za jamii: mwanafunzi anapokanusha sentensi za nafsi ya tatu kuashiria vitendo vya watu mbalimbali nyumbani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapowathamini wenzake wanaposhirikiana katika shughuli za ukanushaji.<br>• Masuala ya kifedha: mwanafunzi anapotumia ukanushaji katika sentensi zinazolenga masuala ya dukani. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya uandishi wa insha anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dukani na yanayofundishwa katika somo la *Mathematics Activities.* |

## 8.0 NDEGE NIMPENDAYE

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Silabi za sauti /mbw, /nd/ na /ny/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kusoma kifungu kifupi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa *(/mbw, /nd/, /ny/)* katika kadi maneno, chati, mti maneno, au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua silabi lengwa,<br>● kutamka maneno aliyosikiliza yenye sauti lengwa; atamke na mwalimu na mwishowe atamke akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu cha hadithi na kutambua sauti lengwa, | Je, matamshi bora hukuzwa kwa njia gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusoma kwa sauti kifungu kilicho na sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>• kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na kujisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli mbalimbali ili kuboresha matamshi yake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujirekodi akisoma hadithi zilizo na maneno yenye sauti lengwa na azisikilize na wenzake ili kutathmini matamshi.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake, kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.
- Heshima: mwanafunzi anapothamini matamshi ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia na kutunza vifaa vya kidijitali katika shughuli inayorejelewa.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposoma kifungu kilicho na sauti *mbw*, *nd* na *ny* kuhusu suala lengwa kwa ufasaha na matamshi bora.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /mbw/, /nd/ na /ny/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa **(**/*mbw*, /*nd*/, /*ny*/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 53 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*),<br>● kusoma kifungu chepesi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu chepesi chenye sauti | Je, ni kwa nini tunasoma kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo kwa ufasaha. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kwa ufasaha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma hadithi kwa ufasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma.
- Ubunifu: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake na kusoma kifungu chepesi kwa ufasaha.

**Maadili**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwa kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia.

**Masuala mtambuko**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora, sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo.
- Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kwa ufasaha na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Tahajia**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tahajia sahihi za maneno katika insha,<br>b) kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno,<br>c) kufurahia kutumia tahajia sahihi katika maandishi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua tahajia sahihi za maneno katika uandishi wa insha kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili kuhusu tahajia sahihi ya maneno katika kifungu kitabuni au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika insha akizingatia tahajia sahihi za maneno katika uandishi,<br>● kurekebisha insha akizingatia tahajia za maneno,<br>● kumsomea mzazi au mlezi insha aliyoiandika kwa kuzingatia tahajia za maneno. | Kwa nini ni muhimu kuendeleza maneno ipasavyo unapoandika chochote? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kujifunza tahajia sahihi za maneno katika insha.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji wa tahajia sahihi za maneno katika insha.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha kwa kuzingatia tahajia za maneno. |
| **Maadili**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapoandika insha akizingatia tahajia sahihi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapojifunza kuandika insha kuhusu suala lengwa akizingatia kanuni za uandishi na tahajia sahihi. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika kuhusu tahajia anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4.Sarufi** | **8.4.1** Matumizi ya Maneno **Hili** na **Haya**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya neno **hili** na **haya** katika kifungu,<br>b) kutumia neno **hili** na **haya** katika kifungu ili kuboresha mawasiliano,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **hili** na **haya** katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya neno **hili** na **haya** *(k.v. jicho hili – macho haya, jino hili – meno haya n.k.)* katika kifungu kwenye chati au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusoma sentensi zinazoonyesha matumizi ya neno **hili** na **haya** katika kifungu akishirikiana na wenzake,<br>● kujaza nafasi kwa kutumia neno **hili** na **haya** akiwa na wenzake,<br>● kuandika kifungu kwa kutumia neno **hili** na **haya** na kujadili na wenzake ili kukitolea maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu alichokitunga ili akitolee maoni. | Ni maneno yapi yanayoambatanishwa na maneno **hili** na **haya**? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojenga msingi wa kujifunza zaidi kuhusu neno **hili** na **haya**.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunzia matumizi ya neno **hili** na **haya**.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotumia neno **hili** na **haya** kurejelea vitu katika mazingira yake. |
| **Maadili:**<br>● Umoja:  mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia neno **hili** na **haya** ipasavyo<br>● Amani: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali na wenzake ili kutambua na kutunga sentensi akitumia **hili** na **haya** kwa utulivu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia maneno lengwa.<br>● Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kutoka jamii mbalimbali kutambua matumizi ya **hili** na **haya**. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vionyeshi na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ndege nimpendaye na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

## 9.0 SOKONI

| Mada | Mada sNdogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Mazungumzo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua suala lengwa linalozungumziwa,<br>b) kuzingatia matamshi bora katika mazungumzo,<br>c) kujieleza kwa ufasaha kuhusu suala lengwa,<br>d) kutumia ishara zifaazo katika mazungumzo,<br>e) kuchangamkia mazungumzo katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua suala lengwa linalozungumziwa kupitia kwa picha kutoka kwenye kitabu, chati, vifaa vya kidijitali pamoja na wenzake,<br>● kuchukua muda wa kufikiri kuhusu suala la kuzungumzia,<br>● kupanga mawazo yake kuhusu suala lengwa na kuandaa hoja za kuzungumzia,<br>● kutamka maneno kwa kuzingatia matamshi yafaayo ya sauti mbalimbali,<br>● kueleza habari ambayo zinaleta maana na zenye kufuatana vizuri,<br>● kupandisha na kushusha sauti panapohitajika,<br>● kutumia ishara mbalimbali zinazohusiana na maelezo yake kuhusu suala lengwa, | Je, unazingatia nini unapozungumza kuhusu masuala mbalimbali? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td><ul><li>kuzungumza na mzazi au mlezi wake akizingatia suala lengwa ili aimarishe mawasiliano.</li></ul></td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<ul><li>Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na wenzake katika kikundi.</li><li>Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza mazungumzo.</li><li>Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo ya kila siku ili kuimarisha mawasiliano.</li><li>Kujiamini: mwanafunzi anapojieleza kwa ufasaha mbele ya wenzake.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<ul><li>Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kwenye kikundi.</li><li>Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali na nyenzo nyinginezo anazotumia kujifunzia.</li><li>Heshima: mwanafunzi anapowasikiliza wenzake darasani na kuheshimu maoni yao.</li></ul></td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<ul><li>Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya mazungumzo na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English Language Activities na Indigenous Language Activities.</li><li>Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la Mathematical Activities.</li></ul></td></tr>
</table>

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2. Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa ufahamu**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi,<br>c) kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha hadithi kwa kuzingatia picha,<br>d) kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya hadithi ili kuimarisha stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusoma kifungu chepesi cha maneno 70- 75 na kutambua msamiati wa suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kutumia msamiati wa suala lengwa ipasavyo katika mawasiliano,<br>● kutabiri kitakachotokea katika kifungu chepesi cha ufahamu kwa kuzingatia picha akiwa na wenzake,<br>● kueleza ujumbe wa kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kueleza mafunzo yanayotokana na kifungu chepesi cha hadithi akiwa na wenzake,<br>● kuthibitisha utabiri wake kuhusu hadithi kama akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kuhusu suala lengwa na kujadili ujumbe. | Je, ni mambo yapi unayozingatia unaposoma kifungu chochote? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofanya utabiri kutokana na picha.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusoma hadithi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma majarida na magazeti kuimarisha stadi ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapowaheshimu wenzake kushirikiana katika kusoma kifungu darasani.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya kifaa cha kidijitali darasani. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya fedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha ya Masimulizi**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha,<br>b) kuandika insha ya masimulizi kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia uandishi wa insha ya masimulizi ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza masimulizi yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali,<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya masimulizi kutoka kwenye masimulizi aliyosikiliza,<br>● kusoma kielelezo cha insha ya masimulizi kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali kuhusu insha ya masimulizi akiwa na wenzake,<br>● kutambua mambo muhimu katika uandishi wa insha katika kielelezo cha insha aliyosoma,<br>● kuandika kisa kifupi kuhusu suala lengwa; kisa hiki kifuate hatua za uandishi: maandalizi, nakala ya kwanza, urekebishaji, nakala safi na kuwasomea wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kisa kifupi kuhusu suala lengwa ili akitolee maoni. | 1. Je, unapenda kusimulia kuhusu nini?<br>2. Je,kisa ulichowahi kusimuliwa kilikuwa na mafunzo gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili vipengele vya uandishi wa insha.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapoandika kifungu cha masimulizi akitumia kifaa cha kidijitali.
- Uwazaji wa kina: mwanafunzi anapotambua mambo yanayotakikana katika uandishi wa insha ya masimulizi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya masimulizi kwa kuzingatia vipengele husika.

**Maadili:**

- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.
- Matumizi ya dawa za kulevya: mwanafunzi anapoandika kisa kifupi kuhusu matumizi ya dawa za kulevya zinazopatikana sokoni.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya uandishi wa insha na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities.*

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1** Matumizi ya: ***Juu ya, Ndani ya na Mbele ya***<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu,<br>b) kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika sentensi,<br>c) kuchangamkia matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** katika matini,<br>● kusikiliza kifungu au wimbo unaotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kutoka kwa mgeni mwalikwa, mwalimu au vifaa vya kidijitali na kutambua matumizi yazo akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kifungu kilichotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kujadili na mwenzake matumizi ya **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya** katika kifungu ili kutolea maoni,<br>● kujaza nafasi ili kukamilisha sentensi zilizotumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake,<br>● kuigiza matumizi ya **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** akiwa na wenzake kwa kutumia vitu anavyomiliki (*k.m*; *Mboga iko ndani ya gunia, Vitabu viko juu ya rafu, Kitabu kiko ndani ya mkoba, Gari liko mbele ya duka),* | Je, ni maneno yapi unayoweza kutumia kurejelea kitu/mtu aliye mahali fulani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumtungia mzazi au mlezi wake sentensi kwa kutumia **juu ya, ndani ya** na **mbele ya** kwa kuzingatia vitu katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za kikundi wanapotungiana sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani y**a na **mbele ya.**
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kusikiliza kifungu au wimbo na vilevile anapofanya zoezi kwa kutumia tarakilishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowatungia wenzake sentensi kwa kutumia **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya.**

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi huku akiyathamini maoni na michango ya wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi na pia anapotangamana na vifaa vya kidijitali.
- Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi kwa utulivu.

**Masuala mtambuko:**

Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoigiza uuzaji na ununuzi akitumia **juu ya**, **ndani ya** na **mbele ya.**

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la sokoni na yanayofundishwa katika somo la *Mathematical Activities*.

## 10.0 TEKNOLOJIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Matamshi Bora**<br><br>*Sauti /mb/, /nz/ na /tw/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua silabi za sauti lengwa katika maneno na kifungu,<br>b) kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa kwa ufasaha,<br>c) kutumia maneno yenye silabi za sauti lengwa ili kufanikisha mawasiliano,<br>d) kufurahia matamshi bora katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua silabi za sauti lengwa (/*mb*/, /*nz*/, /*tw*/) katika kitabu, kadi maneno, chati, mti maneno au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maneno yenye silabi za sauti lengwa yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa akishirikiana na wenzake,<br>● kusikiliza kwa makini sentensi zenye maneno yenye silabi za sauti lengwa zikitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kutambua sauti lengwa | Je, ni kwa nini tunatumia matamshi bora tunapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kwa sauti kifungu kifupi kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kujirekodi akisoma kifungu kilicho na maneno yaliyo na sauti lengwa akisikiliza na wenzake ili kutathmini matamshi,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kifungu kifupi kwa kuzingatia silabi za sauti lengwa kwa matamshi bora. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kutamka maneno yenye sauti lengwa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu na kutambua jinsi alivyotamka sauti lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka maneno yenye silabi za sauti lengwa ipasavyo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojirekodi akisoma kifungu chenye maneno ya sauti lengwa ili waitathmini na wenzake.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kutambua na kutamka maneno yenye silabi za sauti lengwa.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu matamshi ya wenzake wakisikiliza kifungu na kutambua sauti lengwa. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua silabi za sauti lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali akizingatia hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya matamshi bora na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>*Sauti /mb/, /nz/ na /tw/*<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti lengwa katika kifungu chepesi cha hadithi,<br>b) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa sauti inayosikika,<br>d) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo,<br>e) kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kwa ufasaha ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti lengwa (/*mb*/, /*nz*/, /*tw*/) katika kifungu chepesi kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia matamshi bora akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa sauti inayosikika akiwa na wenzake,<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye maneno ya sauti lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno 55 kwa dakika na kwa kuzingatia viakifishi*),<br>● kusoma kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa kwa kuzingatia ishara zifaazo akiwa na wenzake,<br>● kumsomea mzazi au mlezi | Kwa nini ni muhimu kusoma kifungu kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kifungu chepesi cha hadithi chenye sauti lengwa akizingatia matamshi bora,sauti inayosikika, kasi ifaayo na ishara zifaazo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora, kasi ifaayo, sauti inayosikika na ishara zinazofaa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini usomaji wa wenzake darasani.
- Upendo: mwanafunzi anapowashirikisha wengine katika matumizi ya vifaa vya kidijitali darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia.

**Masuala mtambuko:**

- Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma hadithi kutoka kwenye kifaa cha kidijitali inayohusu suala lengwa, awajibike na kuzingatia hatua za kiusalama.
- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposoma hadithi kuhusu suala lengwa pamoja na wenzake kutoka jamii mbalimbali.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kw ufasaha na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.*

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Insha ya Maelezo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vinavyozingatiwa katika uandishi wa insha ya maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo kati ya maneno 85-90 akizingatia kanuni za uandishi,<br>c) kuchangamkia kuandika insha ya maelezo ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo *(k.v wahusika, ujumbe, muundo)* kwenye kitabu, kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza maelezo yakitolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>● kusoma kielelezo cha insha ya maelezo kwenye kitabu, chati au kifaa cha kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kutambua kanuni za uandishi wa insha ya maelezo (*k.v. mwandiko nadhifu, mtiririko)* akiwa na wenzake,<br>● kuandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha ya maelezo na kuwasomea wenzake ili waitolee maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi insha ya maelezo aliyoandika. | Je, unatumia maneno ya aina gani unapotoa maelezo kuhusu kitu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kutambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya maelezo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposikiliza insha ya maelezo kutoka kwa kifaa cha kidijitali.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia vipengele vifaavyo. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi na kuheshimu maoni yao.<br>● Heshima: mwanafunzi anapowatambua na kuwathamini wenzake wakati wa kushiriki katika shughuli za kuandika.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa akizingatia hatua za uandishi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kuandika insha ya maelezo na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities*.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities* |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vitendo**<br><br>**(Vipindi 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vinyume vya vitendo katika matini,<br>b) kutumia vinyume vya vitendo ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitendo na vinyume vyake katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vinyume vya vitendo (*k.v. fungua- funga, keti- simama, twika- tua)* kwenye chati, kitabu au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusikiliza kifungu chenye vinyume vya vitendo kikisomwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali akiwa na wenzake,<br>● kusoma vinyume vya vitendo katika kifungu akiwa na wenzake,<br>● kukamilisha sentensi akitumia vinyume vya vitendo akiwa na wenzake,<br>● kutunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo na kuzijadili na wenzake ili kuzitolea maoni,<br>● kuigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake,<br>● kumtajia mzazi au mlezi vinyume vya maneno alivyojifunza darasani. | Je, unajua vinyume vipi vya vitendo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika vinyume vya vitendo katika sentensi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matumizi ya vinyume vya vitendo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia vinyume vya vitendo. |
| **Maadili:**<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotekeleza shughuli ipasavyo.<br>● Umoja: mwanafunzi anapofanya kazi pamoja na wenzake kikundi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoigiza vinyume vya vitendo vilivyotumiwa kwenye kifungu akiwa na wenzake kutoka jamii tofauti tofauti bila ubaguzi.<br>● Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapotambua vinyume vya vitendo katika kifungu kutoka kwenye kifaa cha kidijitali na kuzingatia hatua za kiusalama. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume vya maneno na anayojifunza katika somo la Kiswahili na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la *English Language Activities* na *Indigenous Language Activities.*<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la teknolojia na yanayofundishwa katika somo la *Environmental Activities.* |

**MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA**

**MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA**

| **Viwango / Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali Na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuwasiliana kwa kuzingatia matamshi bora.** **(***vokali za Kiswahili, konsonanti za Kiswahili;/py/,/vy/,/sh/, /mb/,/nz/,/tw/ /dh/,/th/,/ch/,/mbw/,/nd/ ,ny/*) | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa kikamilifu. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa. | Anawasiliana kwa kuzingatia matamshi bora ya baadhi ya sauti lengwa kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha.** *(kwa kutumia maneno ya heshima na adabu na mazungumzo ya kimuktadha)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno ya heshima na adabu na katika mazungumzo mbalimbali kwa uketo. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia maneno ya heshima na adabu na katika mazungumzo mbalimbali. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha na kikamilifu akitumia baadhi ya maneno ya heshima na adabu na katika baadhi ya mazungumzo. | Anazungumza na kujieleza kwa akitumia baadhi ya maneno ya heshima na adabu na katika baadhi ya mazungumzo kwa kuelekezwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo.** **(***maamkuzi, maagano,kifungu na maagizo*) | Anasikiliza na kujibu maamkuzi, maagano na kifungu na kutoa na kufuata maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa urahisi. | Anasikiliza na kujibu maamkuzi, maagano na kifungu na kutoa na kufuata maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi, maagano na kifungu, na kutoa na kufuata baadhi ya maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo. | Anasikiliza na kujibu baadhi ya maamkuzi maagano na kifungu, na kutoa na kufuata baadhi ya maagizo kwa kuzingatia ujumbe na ishara zifaazo kwa kuelekezwa. |

**MADA: KUSOMA**

| Viwango Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu – kifungu** *( ujumbe, matumizi ya msamiati mwafaka, kutabiri,kueleza mafunzo)* | Anasoma vifungu na kutambua ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo kwa utendeti. | Anasoma vifungu na kutambua ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo. | Anasoma vifungu na kutambua baadhi ya ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo. | Anasoma vifungu na kutambua baadhi ya ujumbe, matumizi mwafaka ya msamiati na kutoa utabiri na mafunzo kwa kiasi. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kikamilifu. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma ufasaha kwa kuelekezwa. |

**MADA: KUANDIKA**

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidi matarajio** | **Kufikia matarajio** | **Kukaribia matarajio** | **Mbali na matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kuandika kwa hati nzuri,** kutenganisha herufi ipasavyo na kuacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika kwa hati nadhifu unaosomeka, anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni kwa wepesi. | Anaandika kwa hati nadhifu unaosomeka, anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika kwa hati usio nadhifu lakini unaosomeka, anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno na pambizoni. | Anaandika hati usiosomeka kwa urahisi, anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo kwenye mistari na anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno na pambizoni kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha.** (*masimulizi, maelezo)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **KuweKuweza kuzingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha.** | Anazingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha kwa utendeti. | Anazingatia alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia baadhi ya alama za uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wa insha. | Anazingatia baadhi ya alama za uakifishaji na uendelezaji wa baadhi ya maneno katika uandishi wa insha. |

**MADA: SARUFI**

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutambua na kutumia maneno mbalimbali katika lugha ya Kiswahili.** **(***yeye, wao, huyo yule, wale, hili, haya, -ake, -ao, eupe, -eusi, -ekundu, juu ya, ndani ya, mbele ya)* | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini kwa kina. | Anatambua na kutumia maneno mbalimbali katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya maneno katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya maneno katika matini kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno.** | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno kwa utendeti. | Anatambua vinyume vya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno. | Anatambua vinyume vya baadhi ya maneno na kuvitumia katika neno kwa kusaidiwa. |

| **Viwango**<br>**Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| *(Vinyume vya vitenzi)* | | | | |
| **Kuweza kutambua na kutumia umoja na wingi wa maneno, vifungu vya maneno na sentensi.** | Anatambua na kutumia umoja na wingi wa maneno kwa utendeti. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa maneno. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa baadhi ya maneno maneno. | Anatambua na kutumia umoja na wingi na udogo wa baadhi ya maneno maneno kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua ukanushaji wa nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi**.<br>*( ukanushaji wa nafsi ya tatu, vinyume vya vitenzi)* | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi kwa wepesi. | Anatambua maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi. | Anatambua baadhi ya maneno yaliyokanushwa katika nafsi ya tatu na vinyume vya vitenzi kwa kuongozwa. |

**KIAMBATISHO : SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI (CSL)**

Katika kiwango hiki, lengo la shughuli ya CSL ni kuambatanisha dhana zilizofunzwa darasani katika masomo mbalimbali na tajriba za maisha halisi ya mwanafunzi. Huwawezesha wanafunzi kuona jinsi mambo waliyojifunza yanavyohusiana na maisha ya kila siku. CSL huwa katika somo la *Environmental Activities*. Mwalimu darasani anatarajiwa kutambua na kuwaelekeza wanafunzi kutekeleza shughuli ya CSL ya darasa zima na jumuishi inayofaa kulingana na umri wa wanafunzi ndani ya shule. Usalama wa wanafunzi unafaa utiliwe maanani wakati wa kuchagua shughuli hii. Zifuatazo ni hatua za shughuli ya CSL jumuishi ambayo inafaa itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula wa shule.

| **Hatua za utekelezaji wa CSL jumuishi** |
|---|
| **1. Maandalizi**<br>• Amua shughuli itakayotekelezwa na wanafunzi.<br>• Tambua umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo mahususi kwa shughuli ya CSL.<br>• Tambua nyenzo hitajika kwa shughuli hiyo (vifaa vinavyopatikana karibu).<br>• Panga shughuli hiyo itekelezwe hatua kwa hatua katika muhula (weka tarehe na saa ya shughuli).<br>• Wasiliana na wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule, walimu na wadau wengine katika jamii ya shule.<br>• Tambua na ukuze vifaa vya kutathminia. |
| **2. Utekelezaji wa shughuli ya CSL**<br>• Wapatie wanafunzi majukumu.<br>• Hakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki katika shughuli hii.<br>• Watazame wanafunzi wanapotekeleza shughuli ya CSL na uweke rekodi ya matokeo.<br>• Tumia kifaa kifaacho cha kutathmini mchakato wa shughuli na matokeo (tathmini kazi ya wanafunzi kutoka mwanzo hadi mwisho).<br>• Tathmini umilisi, maadili na stadi lengwa za masomo. |

**3. Utafakuri wa shughuli ya CSL**

Kuwa na muda wa tathmini binafsi na wanafunzi kuhusu shughuli waliyotekeleza ya CSL jumuishi kwa kujadili yafuatayo:

- Ni nini kilifanyika vyema na kwa nini?
- Ni nini ambacho hakikufanyika vizuri na kwa nini?
- Ni nini kinachoweza kufanywa kwa njia tofauti wakati ujao?
- Ni nini wanafunzi walijifunza?

Kutakuwa na shughuli moja ya CSL kwa mwaka. Masuala makuu ya CSL jumuishi yatatokana na kategoria pana za masuala mtambuko na ujuzi unaolengwa katika masomo mbalimbali. Walimu wanatarajiwa kuwa na masuala tofautitofauti yanayolengwa kila mwaka ili kuwapa fursa wanafunzi kutalii masuala mtambuko mbalimbali. Kunafaa kuwa na uhusiano kati ya stadi za masomo na masuala makuu.

Shughuli ya CSL jumuishi itakuwa ya shule nzima ambapo jamii yote ya shule itahusika (wanafunzi, wazazi/walezi, utawala wa shule na walimu). Wazazi/walezi ni washikadau muhimu katika kupanga na kutekeleza shughuli ya CSL. Ingawa walimu huongoza upangaji na utekelezaji wa shughuli ya CSL, wanafunzi watatarajiwa kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima.

Shughuli hii ya CSL hutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili mbalimbali. Mwalimu anatarajiwa kulenga umilisi na maadili tofautitofauti.

**Tathmini ya shughuli ya CSL**

Tathmini ya CSL jumuishi italenga vipengele 3 ambavyo ni: stadi kutokana na masomo mbalimbali yatakayojumuishwa katika shughuli hii, umilisi wa kimsingi uliokuzwa na maadili yaliyokuzwa. Tathmini inafaa kulenga mchakato mzima wa utekelezaji na matokeo ya mwisho ya shughuli. Mwalimu atatathmini wanafunzi katika vikundi akitumia vifaa mbalimbali kama vile ratiba ya ukaguzi, orodha hakiki, kiwango cha ukadiriaji na vifaa vingine faafu vya tathmini.